SportPesa
TZS. 499,059,740
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wakulima** wa korosho watwangana makonde wakigombea viuatilifu

UKURASA 3




**Benzema ampigia saluti Vinicius Jr**

UKURASA 21

Nipashe
Jumanne Septemba 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580703
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Wateule msinichukulie poa

**• Asema** wengine wakae mguu sawa, atoa agizo kuhusu wamachinga...

*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi mbalimbali mara baada ya tukio la uapisho lililofanyika katika viwanja vya Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA NA IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**
**TAMWA YAFAGILIA UTEUZI WANAWAKE 2**
CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimempongeza...

**UKURASA WA 5**
**MATUMIZI PLASTIKI MARUFUKU KWENYE TAASISI ZA SERIKALI**
SERIKALI imepiga marufuku matumizi ya kamba za plastiki, matumizi...

**UKURASA WA 8**
**SHULE ZA CCM ZAFUNGWA KISA KUKOSA WANAFUNZI**
SHULE za sekondari nane kati ya 58 zinazomilikiwa na Jumuiya ya...

## Kazi ya Rais kupigia debe utalii yaanza kuleta fursa

UKURASA 4



## Vikwazo kwa Makamba, Mbarawa, Kijaji hivi

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA: TUTASONGA MBELE AFRIKA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## ...Machinga wapangwe, wasibugudhiwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaagiza wakuu wa mikoa kuchukua hatua za kuwapanga vyema wajasiriamali wadogo maarufu kama 'machinga' bila uonevu.

Akizungumza kwenye uapisho wa mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ikulu jana, Rais Samia alisema serikali imetoa fursa kubwa kwao kufanya biashara ili kujipatia kipato.

"Watu hawa wamekuwa wakifanya kazi kwenye maeneo tofauti tofauti, wakuu wa mikoa wanawapanga, wakuu wa wilaya wanawapanga, lakini pia watu wamepumzika kiasi ambacho watu hawa sasa wameenea kila mahali mpaka kwenye maduka wao wanaziba, wanauza mbele."

"Mpaka sasa wenye maduka baadhi yao wamepata mtindo wa kutoa bidhaa zao ndani na kuwapa machinga kuuza kwasababu watu hawaingii ndani, lakini kitendo hiki kinatukosesha kodi kwasababu machinga halipi kodi, lakini mwenye duka anatakiwa kulipa," alisema.

Aliwataka wakuu hao kuchukua hatua za kuwapanga vyema na kuonya anayoyaona kwenye runinga ya ngumi, kupigana, kufukuzana, kuchafuliana na vitu kumwagwa, hataki kuyaona.

Alisema hatua hizo zichukuliwe vizuri na kuwapanga vyema bila kuudhi wenye maduka wala machinga.

"Niwaombe sana ndugu zangu wakuu wa mikoa mnaonisikia na wale wanaonisikia kupitia runinga wachukue hatua zinazostahiki bila kuleta vurugu, fujo na uonevu," alisema.

Alitoa wito kwa machinga au wajasiriamali wafuate sheria na kanuni zilizopo na wajitahidi kufuata yale wanayopangiwa na wakuu wa mikoa na wilaya.

Kuhusu viongozi walioapishwa, Rais Samia aliwataka walioapishwa kufanya kazi kwa umahiri mkubwa katika maeneo yao kwa lengo la kutoa huduma stahiki kwa wananchi nasi vinginevyo na yeye ataendeleza kazi ya marekebisho.

"Nimeanza na mabadiliko kwenye muundo wa wizara mbili iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo sasa inabaki kuwa Sanaa, Utamaduni na Michezo na nimechukua Habari nimeipeleka iliyokuwa mawasiliano na Teknolojia ya Habari."

"Nimefanya hivyo kwasababu Wizara ya Habari, Teknolojia ya habari ili iwe kamili yale maneno habari yote yawe huko na nadhani ikikaa hivi yatakaa vizuri, kilikuwa kilio cha muda mrefu cha watu wa sekta ya habari walipenda idara ile iwe pale," alisema.

Alisema wizara hiyo ni nzito kidogo ingawa utekelezaji wa mambo yake ulikuwa unachukuliwa kwa wepesi na kumtaka Dk. Ashatu Kijaji kujipanga vizuri.

# Samia: Msinichukulie poa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaonya viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri, kwamba wasichukulie ukimya na utulivu wake kama udhaifu, huku akisisitiza kuwa atafoka kwa kalamu.

Aidha, amesema katika kipindi cha miezi sita ya urais wake alijaribu kuwa mkimya na mtulivu na kuzisoma wizara zote zinavyoendeshwa na mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu na manaibu makatibu wakuu.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akiwaapisha mawaziri wanne ambao ni Dk. Stergomena Tax, kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), January Makamba, Waziri wa Nishati, Dk. Ashatu Kijaji, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, hafla iliyofanyika Ikulu, Chamwino.

"Kama nilivyosema hapa nilipofika nimeweka koma sijaweka nukta, adjustment (mabadiliko) hizi zinaendelea kwa hiyo tutakavyoendelea wizara hii nayo nitaifanyia marekebisho nao watakuja kuapa mbele yenu," alisema.

Rais Samia alisema mabadiliko, matengenezo, marekebisho aliyofanya juzi usiku yataendelea kufanyika kutokana na jinsi alivyoona utendaji wa mawaziri na viongozi wengine, kwamba serikali yake itaendeshwa kwa matendo makali na si maneno.

Rais Samia alisema wengine walichukulia ukimya na utulivu wake kama njia ya wao kufanya kazi na kuonyesha kwamba wanaweza kufanya kazi.

"Lakini nataka niwaambie kipindi cha miezi sita nilikuwa najifunza, nilivyokuwa Makamu wa Rais nilikuwa na nyinyi, lakini sikupata fursa ya ndani ya kujifunza utendaji wa wizara."

"Nilikuwa najifunza sasa nimeona jinsi ya kwenda na nyie, katika uongozi kuna mbinu nyingi na tulivyokuwa tunafundishwa mambo ya uongozi tulifundishwa kuna style (mtindo) ya karoti na stick, kwa hiyo unaweza kutumia moja katika hizo au kwa pamoja."

"Nimejichagulia njia yangu nataka niwaambie kwamba tunapoendelea huko serikali yetu itaendeshwa kwa matendo makali na sio maneno makali."

"Ninaposema matendo makali wala siyo kupigana mikwaju au mijeredi ni kwenda kwa wananchi na kutoa huduma inayotakiwa kila mtu kufanya wajibu wake."

"Msinitegemee kwa maumbile yangu haya pengine na malezi yangu kukaa hapa nianze kufoka wee, waa... waa..., nahisi si heshima na kwasababu nafanya kazi na watu wazima wanaojua jema na baya ni lipi ni imani yangu kwamba tunapozungumza tunaelewana na kila mtu anajua afanye nini kwenye wajibu wake."

"Msitegemee mimi kuanza kufoka ovyo, kufokea watu wazima wenzangu, nitafoka kwa kalamu, katika kipindi cha miezi sita hiki kuna watu walichukulia hii serikali poa, serikali 'cool' kwa hiyo watu wakafanya wanayoyataka," alionya.

Rais Samia aliongeza: "Kuna mambo mengi ya kurekebisha, lakini katika kipindi hicho pia hao hao niliowataja mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu, manaibu walinisoma mimi pia na wakati mimi nawasoma wao na wao walikuwa wananisoma mimi, kama nilivyosema kati yao walichukulia ukimya na utulivu wangu kama udhaifu na wakaanza kufanya yanayo wapendeza".

Alibainisha kuwa jana ameapisha mawaziri wanne na mwanasheria mmoja na anajua kwamba wizara moja ambayo amepangua muundo wake ilitakiwa uongozi wake uwapo kuapa upya kwasababu sio wizara waliyokula kiapo awali.



Mawaziri wanne na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walioteuliwa wakila kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. i. **PICHA: IKULU**

## Mpango, Majaliwa, Ndugai wawafunda mawaziri wapya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI wakuu serikalini wameeleza namna mawaziri walioteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan juzi, walivyo na kibarua cha kuwatumikia Watanzania kwenye sekta mbalimbali.

Mawaziri ni Dk. Stergomena Tax wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT); January Makamba wa Nishati; Dk. Ashatu Kijaji wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Prof. Makame Mbarawa wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mbali na mawaziri mteule mwingine wa Rais Samia ambaye pia aliapishwa jana ni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi.

Akizungumza kwenye uapisho wa viongozi hao, Spika wa Bunge Job Ndugai, alisema Bunge ni kama chuo watu wamekuwa wakipanda na wengine kushuka na wengine wakipotea.

Alisema Prof. Mbarawa wizara aliyopewa ni kubwa na imebeba sehemu kubwa ya bajeti ya serikali na kuahidi Bunge litamsaidia.

"Dk. Tax umepewa kibubu nyeti kabisa cha ulinzi Mungu akutangulie, ni imani kubwa sana ya Rais kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri wa Ulinzi umeaminika sana, Dk. Ashatu kwenye teknolojia ya habari dunia ya sasa ipo hapo kwako utusaidie sana, mabadiliko ya teknolojia ni muhimu sana kwenye nchi yetu na hasa kwenye kupunguza gharama za uendeshaji wa serikali," alisema.

Kuhusu Nishati, Ndugai alisema ni eneo la kipekee na nyeti na kwamba wakati Makamba akiwa Mwenyekiti wa Kamati alifanya kazi nzuri.

"Eneo la gesi hapa katikati hatukulipa heshima yake ni eneo la utajiri lazima eneo la gesi lifanyiwe kazi na nchi ipate mapato ya kutosha, pia Liganga Mchuchuma ni moyo wa nchi limezungumzwa sana huko nyuma hebu tukazalishe umeme pale, tukifanikiwa tutafika mbali, ukifanya kazi vizuri (Makamba) unatutoa hapa tulipo," alisema. Naye, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alimtaka Waziri Makamba kusimamia miradi mikubwa kwenye sekta yake isikwame hata kidogo.

"Mradi wa umeme vijijini,tupa jicho kwa watendaji wa TANESCO, angalia maeneo ambayo gridi ya umeme haijafika,Mbarawa kawasimamie makandarasi na TANROADS ,huko kwenye usafiri wa majini miradi tuliyoahidi, itekelezwe na kukamilika," alisema.

Hata hivyo, alisema Mwanasheria Mkuu anaifahamu serikali kuna kero nyingi sana anaamini atasaidia kukwepa matatizo mengi waliyokuwa nayo kwenye mikataba mbalimbali.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema wao kama wasaidizi wa Rais wanalo jukumu la kujifunza mwelekeo na matakwa ya Rais kwenye eneo waliomo ili kila mmoja awajibike kikamilifu.

"Mawaziri wenzangu karibuni tumewapokea kwa mikono miwili, naamini tutakaa pamoja kufanya mapitio ya maeneo mengine, lakini katika kipindi hiki niwasihi pale ambapo mtakabidhiwa majukumu na wale waliowatangulia mtaendelea kuzisoma na kuzielewa vizuri wizara zenu ili tuweze kufanya kazi kwa weledi, niendelee kukuahidi tutaendelea kuwajibika ipasavyo kwa weledi na kwa uaminifu mkubwa ili kuhakikisha serikali yako inatoa huduma, inatekeleza malengo yako na kuwafikia Watanzania popote walipo," alisema Waziri Mkuu.

HABARI KITAIFA

# Vikwazo kwa Makamba, Kijaji, Mbarawa hivi

**Na Gwamaka Alipipi**

JUZI usiku Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri, kwa kuwaondoa mawaziri watatu na kuwateua wapya.

Miongoni mwa mawaziri walioondolewa ni aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dk. Merdad Kalemani, aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho.

Mawaziri wapya walioteuliwa katika uteuzi huo ni January Makamba ambaye anakuwa Waziri wa Nishati, Dk. Ashatu Kijaji ambaye anakuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Profesa Makame Mbarawa, anayekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Dk. Stergomena Tax, ambaye anakuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Hata hivyo, uteuzi wa mawaziri hao unakwenda kuwapa kazi kubwa za kiutendaji, kwamba wanakwenda kukutana na vikwazo kadhaa katika kutatua changamoto mbalimbali katika wizara zao.

**JANUARY MAKAMBA**

Mojawapo ya changamoto iliyopo mbele yake ni kuhakikisha anamaliza tatizo la kukatika umeme ovyo, hali ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wananchi maeneo mengi kwa muda mrefu.

Mbali na hilo, Makamba atatakiwa kuhakikisha miradi mikubwa ya kimkakati inakamilika kwa wakati ukiwamo wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere 'Stiglers Gorge' kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa uhaka ili uweze kujiendesha.

Kadhalika, Makamba anakabiliwa na mtihani wa kumaliza kilio cha wakazi wengi wa vijijini kwa kuhakikisha umeme unawafikia.

Mbali na hilo, pia atakuwa na kibarua cha kuhakikisha anafufua miradi ya gesi, katika mikoa ambayo imegundulika kuwa na rasilimali hiyo kama Mtwara. Pia kuhakikisha nchi inanufaika na nishati hiyo kwa matumizi ya ndani pamoja na kuuza nchi za nje.

Waziri Makamba pia atakuwa na kazi ya kuhakikisha anasimamia kwa karibu nishati ya mafuta ikiwamo upatikanaji na biashara yake kwa ujumla.

Makamba vilevile atakuwa na mtihani wa kusimamia uendelezaji wa kutafuta mafuta kwa ajili ya uchimbaji katika siku za usoni pamoja na utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga.

Waziri Makamba atawajibika pia kusimamia na kuwawajibisha watumishi na watendaji wa TANESCO kutokana na utendaji kazi wa kimazoea unaokwamisha utoaji huduma nzuri kwa wananchi.

**MAKAME MBARAWA**

Waziri Mbarawa amekabidhiwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ambayo ndiyo uti wa mgongo kwa nchi hususani kwenye usafirishaji wa mazao ya kilimo ndani ya nchi hata kwenda nchi za nje.

Profesa Mbarawa licha ya kuwahi kuiongoza wizara hiyo katika Serikali ya Awamu ya Tano, atakuwa na kibarua kikubwa cha kuhakikisha miradi ya barabara inakwenda kukamilika kwa wakati hususani maeneo ya vijijini ambako barabara za lami zimekuwa changamoto.

Aidha, Profesa Mbarawa atakuwa na kazi ya kuhakikisha ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) unakwenda kukamilika kwa wakati na kufungua fursa za kiuchumi.

Pia, Profesa Mbarawa atakuwa na mtihani wa kuhakikisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) linajiendesha kwa faida, halipati hasara tena kama ilivyoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye ripoti mbalimbali.

Wizara yake pia imo katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, hivyo atakuwa na jukumu la kuisimamia ikamilike.

**ASHATU KIJAJI**

Dk. Kijaji amekabidhiwa wizara yenye changamoto nyingi ikiwamo wizi, utapeli katika mitandao ya simu. Matukio ya wananchi kutapeliwa katika mitandao ya simu yamekuwa yakiongezeka kila wakati.

Kadhalika, atakuwa na kazi ya kuhakikisha anaisimamia sekta ya habari hususan kuondoa malalamiko ya vyombo vya habari kupewa adhabu kuwa, ikiwamo kufungiwa.

Waziri Kijaji pia atakuwa na jukumu la kusimamia maendeleo ya TEHAMA kwa kuzingatia kuwa ni sekta muhimu katika dunia ya leo.

Kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza katika kampuni za simu nchini, hilo linampa kazi ya ziada ya kuhakikisha kuwa ufumbuzi unapatikana

**STERGOMENA TAX**

Ni mwanamke wa kwanza Tanzania kuongoza wizara nyeti ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kabla ya kukabidhiwa wizara hiyo alikuwa ni Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC).

Mojawapo ya changamoto atakayokutana nayo na kuhitaji kuitatua ni kuhakikisha Shirika la Uzalishaji Mali la Suma JKT linajiendesha kwa faida na kuleta tija katika uchumi wa nchi.

Waziri Tax atakuwa na jukumu kubwa la kuisimamia wizara hiyo kwa kusikiliza, kufuatilia na kutatua changamoto za wapiganaji na makamanda wa jeshi letu.



## Wakulima korosho watwangana

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKATI serikali ikitoa bure viuatilifu vya kupulizia kwa ajili ya kuua wadudu kwenye mikorosho kwa wakulima wa mikoa inayolima zao hilo, wakulima wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wameripotiwa kuanzisha vurugu na kutwangana makonde wakati wakigawana dawa hizo.

Hayo yamebainika kufuatia taarifa kutoka kwenye maeneo ya vyama vya ushirika vya msingi vilivyopo katika Kata za Mlingoti Mashariki, Ngapa, Lukumbule Tinginya na Kata ya Mchangani.

Taarifa hizo ambazo zimetolewa na baadhi ya viongozi wa serikali na viongozi wa siasa, zinaeleza kuwa baadhi ya maeneo wananchi ambao siyo wakulima wa korosho walivamia maghala usiku na kuyavunja kisha kugawana dawa hizo na kwenda kuuza kwa bei ndogo kwa wakulima.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakulima wa zao hilo walisema serikali ilipaswa kuweka kiasi kidogo cha fedha wakati wa kugawa dawa hizo, lakini kwa utaratibu wa kugawa bure imewanufaisha wakulima hewa.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Mussa Manjaule, alithibitisha kuwapo kwa matukio hayo. Alisema mbali na upungufu wa dawa hizo, lakini wangefuata maelekezo na utaratibu wa ugawaji wake, kwamba matukio hayo yasingejitokeza.

Alisema hadi sasa TAMCU kimepokea tani 1,108 za dawa ya unga aina ya Sulpher ambazo zimepokelewa pamoja na lita 179,701 za dawa ya maji zimepokelewa na kusambazwa kwa wakulima.

Alisema dawa hizo ni kati ya mahitaji ya mgawo wa tani 2,730 za mahitaji halisi ya dawa za unga na viatilifu vya dawa ya maji lita 58,312 ambavyo vilihitajika kwa msimu wa mwaka huu.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa AMCOS, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Mlingoti Mashariki, Said Makochela, alisema wao wanafuata taratibu na maelekezo yaliyotolewa na viongozi wa serikali na chama kikuu ikiwa ni pamoja na kuita majina ya wakulima ambao huuza korosho zao katika maeneo yao wakiwa wanawashirikisha maofisa ugani.

Alisema kumekuwapo na vijana kutoka vijiweni ambao wamekuwa wakifika kwenye maeneo ya kugawa viuatilifu na kufanya fujo, kupora dawa.




# Kazi ya Rais kuutangaza utalii yaanza kuleta fursa

**Na Elizabeth Zaya**

MPANGO wa kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia kipindi maalum kinachorekodiwa na Rais Samia Suluhu Hassan maarufu kama 'Royal Tour' kwenye vivutio mbalimbali vya utalii nchini, umewavuta mawakala zaidi ya 30 kutoka Marekani, Ufaransa na Lithuania.

Mawakala hao wanatarajia kuja nchini Novemba 23, mwaka huu kwa lengo la kutembea katika maeneo mbalimbali yenye vivutio vya utalii kwa ajili ya kuwekeza.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Kimataifa inayojishughulisha na masuala ya utalii(KITS), Francis Malugu, alisema mawakala hao wamevutiwa kuja nchini baada ya kupata taarifa ya kipindi hicho cha Royal Tour kinachorekodiwa na Rais Samia.

Kwa mujibu wa Malugu, ujio wa mawakala hao umeratibiwa na kampuni hiyo ya Utalii ya KITS na kuishirikisha Bodi ya Utalii Tanzania (TTB). "Baada ya kuona jitihada za Rais kuitangaza Tanzania kupitia kipindi anachorekodi, tuliwataarifu mawakala wa utalii katika vyama vya utalii duniani ambavyo KITS ni mwanachama wake, na zaidi ya mawakala hao 30 waliomba na kuthibitisha kuja nchini Novemba mwaka huu, huu ni mwanzo mzuri na tunapongeza hatua hii ya Rais kutangaza vivutio na tunaona kazi hii imeanza kuzaa matunda," alisema Malugu.

Alisema kipindi hicho kilichorekodiwa na Rais Samia, kitasaidia kukuza uwekezaji, kuvutia utalii pamoja na kurahisisha shughuli za utangazaji wa vivutio vya utalii vya Tanzania katika nchi mbalimbali duniani.

"Na itasaidia pia kuifanya dunia kuitambua Tanzania kama sehemu ya mahsusi ya asili ya dunia ambayo kila mpenda utalii atatamani kuitembelea na tunaamini kupitia njia hiyo, itachangia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa nchi kupitia watalii, wawekezaji na wafanyabiashara," alisema Malugu.

Kaimu Mkurugenzi wa Masoko wa TTB, Felix John, alisema kutembelewa na mawakala hao ni fursa kubwa kimkakati katika kufanikisha lengo la kutangaza vivutio vilivyopo nchini kwa kuvutia watalii wasiopungua milioni tano ifikapo mwaka 2025 na kuliingizia taifa dola za Kimarekani zisizopungua bilioni sita.

"Kimkakati hilo ni jambo muhimu kwetu na tunapongeza KITS na wadau wengine wanaoendelea kuhamasisha utalii wetu katika nchi mbalimbali duniani," alisema John.

Rais Samia alianza kurekodi kipindi hicho maarufu kama 'Royal Tour' kwenye maeneo mbalimbali ya vivutio vya utalii na uwekezaji, sanaa na utamaduni vilivyopo nchini Agosti 28, mwaka huu kwa lengo la kuitangaza Tanzania kimataifa.

Kazi hiyo ya kurekodi kipindi hicho maalum ilianzia visiwani Zanzibar na kufuatiwa na Tanzania Bara.




Wakurugenzi wa kampuni ya Puma Energy Tanzania, Selcom Tanzania, Sanlam pamoja na Tan management Insurance Brokers Limited, wakionyesha mkataba wa makubaliano waliosaini jijini Dar es Salaam jana. Mkataba huo unahusu kuanzisha huduma ya bima ya ajali na maisha ambayo italenga kuinua sekta ya soko la bima Tanzania. Kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Sanlam Tanzania, Khamis Suleiman, Mkurugenzi Mtendaji wa Selcom Tanzania, Sameer Hirji, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mafuta ya PUMA Energy Tanzania, Dominic Dhanah na Mkurugenzi Mtendaji wa TanManagement Insurance Brokers Limited, Mohammed Jaffer. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yafagilia uteuzi mawaziri wanawake 2

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuteua wanawake wawili katika Baraza la Mawaziri, uteuzi uliofanyika juzi.

Katika uteuzi huo, Rais Samia alimteua Dk.Ashatu Kijaji kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Dk. Stergomena Tax, kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

"TAMWA tunampongeza Rais Samia, kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, kumteua mwanamke kushika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Uteuzi huo unaonyesha dhahiri kuwa wanawake wanaaminika na wana uwezo wa kuleta mabadiliko katika nyanja zote, kisiasa, kiuchumi na kijamii, uteuzi huu unafanya idadi ya mawaziri wanawake kufikia saba kutoka watano walioteuliwa awali" alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben.

Alisema TAMWA wanaamini kuwa, ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi ndiyo nguzo muhimu ya kuleta usawa na ni chanzo cha kuleta mabadiliko chanya katika jamii, ambayo yanatokana na usawa, haki na uwajibikaji.

"Rais Samia, ameonyesha lile ambalo lilidhaniwa haliwezekani kwa kuwaweka mawaziri wanawake katika wizara nyeti kama ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, pia kwa kuendelea kuteua mawaziri wanawake, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na makatibu tawala," alisema Dk. Reuben.

"Hakika Rais amevunja dhana ya kuwa wanaume pekee ndiyo wenye uwezo wa kushika wizara hii, na kwa hili tunategemea Dk. Tax hatatuangusha, bali atasimamia vyema nafasi hiyo na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika masuala ya ulinzi na usalama, kwa kuwa ana uwezo na upeo."

Pia, TAMWA ilimpongeza Rais Samia kwa kusikiliza kilio cha wanahabari kwa kuunganisha Wizara ya Habari, Mawasiliano na ile ya Teknolojia ya Mawasiliano, kuwa moja.

"Hatua hiyo itasaidia wadau wa habari kufanya kazi kwa ufanisi na wepesi zaidi kuliko hapo awali. Tunaamini kuwa ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi na katika ngazi za uamuzi ndicho chanzo cha haki, usawa na uwajibikaji na maendeleo ya nchi," alisema Dk. Reuben.

# 16 mbaroni madai ya uhamiaji haramu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIA 16 wa Ethiopia wakiwamo watoto 11 wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuingia nchini bila kufuata taratibu ikiwamo kuwa na vibali vinavyowapa uhalali wa kuingia.

Aidha, Jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja, Yohana Adam (30), mkazi wa Mji wa Kasumulu wilayani Kyela ambaye ndiye alikuwa anawasafirisha wahamiaji haramu hao kuwapeleka nchi jirani ya Malawi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watu hao walikamatwa juzi katika Kijiji cha Namba One kilichopo Kata ya Isongole wilayani Rungwe.

Alisema walikuwa wanasafirishwa kwa kutumia gari ndogo aina ya Toyota Noah yenye namba za usajili T.351 DBD ambayo ilikuwa inaendeshwa na mwenyeji wao Adam.

"Lakini pia kwenye hili kuna watu sita ambao wanashirikiana na huyu msafirishaji kwenye hiyo kazi, nawataka wajisalimishe mapema kabla hatujawafuata sisi, hii biashara ina madhara makubwa sana kwa taifa letu," alisema Matei.

Kamanda Matei aliwataja wahamiaji hao waliokamatwa ni Adson Tagala (18), Adino Ozrey (18), Abduke Tibeso (25), Adam Kibromo (25) na Tamar Mohamed (20) ambao ndio vijana pekee kwenye msafara huo na wanaobaki wote ni watoto.

Aliwataja pia watoto waliokamatwa ni Molukan Adana (15), Shetu Yonas (13), Tamarigid Yadere (11) Erimia Makneko (15), Joseph Ganamo (13), Falack Kabson (17) na Tigabo Maalasa (15)..

Aliwataja watoto wengine ni Yonas Fikerey (14), Masala Adana (15), Tashari Tamaske (14) na Thomascan Tashara (17).

Kamanda Matei alisema wahamiaji hao walikuwa wanasafirishwa na mwenyeji wao huyo kutoka Kenya kwenda Afrika Kusini kupitia Malawi kwa kuingilia mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela.

Aliwataka madereva wa magari nchini hasa vijana kuacha kufanya kazi hiyo ya kuwasafirisha wahamiaji haramu hao akidai kuwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria na kwamba adhabu yake ni kutaifishwa kwa gari na mhusika kutozwa faini kubwa.

# Kamba za plastiki zapigwa marufuku taasisi za serikali

**Na Ashton Balaigwa,** KILOSA

SERIKALI imepiga marufuku matumizi ya kamba za plastiki, matumizi ya vifungashio vya plastiki ikiwamo magunia kwenye taasisi zake, badala yake watumie vifungashio vinavyotokana na mkonge unaozalishwa hapa nchini.

Maamuzi hayo ya Serikali yamekuja baada ya kubainika kamba hizo zinaleta athari kwa afya wa binadamu pamoja na uharibifu wa mazingira hapa nchini.

Agizo hilo limetolewa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kupitia hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika mkutano wa pili wa wadau wa sekta ya mkonge hapa nchini, ulioshirikisha wakulima, wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi na wadau wanaolima zao hilo nchini.

Waziri Mkuu Majaliwa aliiagiza Wizara ya Kilimo, kutoa tamko la kisera kwa ajili ya kuzuia matumizi ya kamba za plastiki nchini, ambazo zimebainika nyingi ni bandia na zinazalishwa kwa njia za panya.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko ya muda mrefu kuhusu kuwapo kwenye soko kwa kamba hizo bandia za plastiki ambazo zimetengenezwa na viwanda bubu hapa nchini.

Hivyo aliiagiza Shirika la Viwango (TBS) kudhibiti kamba hizo katika soko na Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) kuhakikisha inazipiga marufuku kwa kuwa ni tishio kwa mazingira.

Alisema pamoja na malalamiko hayo lakini matumizi ya mifuko ya plastiki imekuwa pia ikisababisha serikali kupoteza mapato yanayotokana na kodi.

Majaliwa alisema lengo la Serikali ni kuinua kilimo cha mkonge kwa kuongeza uzalishaji kutoka tani 37,000 za hivi sasa hadi tani 120,000 ifikapo mwaka 2025.

Waziri Mkuu Majaliwa aliagiza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ikabidhi kwa Bodi ya Mkonge Tanzania, mashamba yote yaliyofutwa na Rais Samia Hassan Suluhu kwa ajili ya kugaiwa wananchi.

# Tabianchi inavyotishia Milima Tao Mashariki

**Na Felix Andrew**

WANASAYANSI wa ndani na nje wametabiri kuwa katika nusu ya karne ijayo, joto litaongezeka na kiasi cha mvua kitabadilika katika maeneo mengi nchini ikiwa ni sehemu ya matokeo ya mabadiliko ya tabianchi.

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na wanasayansi wa kitaifa na kimataifa umeripoti kuwa, kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita, joto limeongezeka kwa nyuzi joto 0.58 katika Milima ya Usambara iliyoko Wilaya za Muheza, Korogwe na Lushoto mkoani Tanga.

Mmoja wa wanasayansi aliyeshiriki katika utafiti huo, Dk. William Newmark, kutoka Jumba la kumbukumbu ya Historia ya Asili la Utah, nchini Marekani, alisema: "Ingawa ongezeko la joto la nusu digrii kwa zaidi ya miaka 30 linaweza kuonekana kuwa dogo kabisa, athari zake kwa spishi na idadi ya ndege ni kubwa sana."

Kati ya miaka ya 2018 na 2021, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ikishirikiana na Amani Friends of Nature, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Tume ya Sayansi na Teknolojia, Kikundi cha Uhifadhi wa Misitu Tanzania na Jumba la kumbukumbu ya Historia ya Asili la Utah, Marekani; kwa ufadhili wa shirika la JRS- Biodiversity Foundation, walitekeleza mradi wa kutathmini athari za mabadiliko ya tabianchi kwa ndege na vipepeo wachavushaji kwenye milima ya Usambara na Uluguru.

Sehemu ya mradi huu ulifanya marudio ya utafiti wa ndege katika milima ya Usambara, utafiti ambao uliwahi kufanyika takribani miaka 39 iliyopita, kwenye mwinuko ulioanzia mita 300 hadi mita 2100.

Utafiti huu ulibaini kuwa spishi nyingi za ndege zilizopo katika safu za milima hii zimehamia katika ukanda wa juu zaidi ilikukwepa hali ya joto inayoongezeka ukanda wa chini wa milima.

Hata hivyo, mwanasayansi huyo anasema"kuhama kwa spishi hizi kuelekea katika maeneo ya juu ya mwinuko, hakuendani na kasi yaongezeko la joto, na mbaya zaidi makazi ya spishi nyingi yametoweka na kupelekea spishi nyingi za ndege kushindwa kuvuka maeneo wazi kati ya msitu na msitu".

Misitu iliyopo katika Milima ya Usambara pia imeonekana kutenganishwa na maeneo makubwa ya wazi ambayo ndege wengi hawawezi kuvuka. Aidha, utafiti wa ziada katika Milima ya Usambara pia umebaini kuwa kiwango cha kuzaliana na ukuaji wa baadhi ya spishi za ndege kimepungua kwa zaidi ya theluthi mbili ya spishi zote za ndege kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita, na kushuka huku kunahusishwa na kuongezeka kwa joto.

Wanasayansi hao wanapendekeza kuwa serikali kwa kushirikiana na wananchi ianzishe shoroba kwa kuhuisha msitu kati ya misitu mikubwa na midogo iliyo karibu na Milimaya Tao la Mashariki mwa Tanzania ili kuruhusu viumbe hawa kupata urahisi wa kuweza kuepuka joto linaloongezeka.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

TRAINING INSTITUTE

KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 18/10/2021. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/09/2021.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia (A,B,C,D)
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa au kusoma nchini.
vi. Asiwe na mchoro au tojo ( visible tattoo) kwenye sehemu za mwili zinazoonekana.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV
v. Kwa wageni, vibali vya kukaa au kusoma Tanzania

**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543 Dar**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**

216455502



PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com
website:www.airtanzania.com

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Shughuli za serikali zifanyikie Dodoma*

**SERIKALI** ya awamu wa tano iliamua kuvunja mfupa ulioshindikana kwa muda mrefu wa kuhamishia shughuli zake na ofisi kwenye makao makuu ya nchi ambayo yapo jijini Dodoma

Hata hivyo, pamoja na serikali kuhamia Dodoma na kutungwa kwa sheria ya kuhalalisha uamuzi huo, inaelezwa kuwa bado wapo baadhi ya mawaziri na watendaji wa serikali wanaoendelea kusafiri hadi jijini Dar es Salaam kufanya mikutano, semina na makongamano.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, ndiye aliyeibua sakata hilo, kwamba magari ya viongozi wa serikali yamekuwa 'yakitiririka' kila wakati kuelekea jijini Dar es Salaam kutokea Dodoma, baada ya siku mbili yanarudi Dodoma.

Kwa mujibu wa Spika Ndgai, hatua hiyo inaongeza gharama za matumizi kwa serikali kwa kuwa kiongozi akielekea jijini Dar es Salaam kutoka Dodoma kuna gharama za malipo mbalimbali zikiwamo posho kwa wasaidizi wake, dereva na wao wenyewe.

Tunakubaliana na kauli hiyo ya Spika kuwa ni kweli mawaziri na watendaji kwenda jijini Dar es Salaam kila mara ni kunaiongezea serikali gharama, kutokana na fedha wanazotumia ambazo ni kodi ya wananchi. Kimsingi, yapo maeneo mengi ambayo yanahitaji kuboreshwa, kuanzia kwenye miundombinu ya afya, elimu, maji, barabara na kwingine ili Watanzania waweze kupata huduma bora.

Hivyo, tunadhani kuna haja kwa viongozi hao kuipunguzia serikali mzigo kwa kufanya shughuli za kiserikali wakiwa makao makuu ya nchi badala ya kusafiri hadi jijini Dar es Salaam, hali ambayo inachangia kuongeza gharama zisizo za lazima.

Kama ambavyo serikali iliamua kuhamia Dodoma, basi tunaona ni vyema shughuli zote ziwe zinafanyikia kwenye makao makuu ya nchi, lakini kwa Dar es Salaam iwe kwa ulazima. Tunaamini kwamba, njia hiyo itasaidia kuipunguzia serikali gharama ili fedha ambazo zingetumiwa na mawaziri na watendaji hao katika safari za Dar es Salaam, zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo na huduma kwa wananchi.

Si kwamba mawaziri na watendaji wasiende Dar es Salaam, bali kuwe na jambo maalum ambalo linawalazimu kufanyia nje ya Dodoma, lakini vinginevyo, tunadhani ni muhimu kila kitu kuishia makao makuu ya nchi.

Ushauri wetu unabaki kwenye umuhimu wa kubana matumizi ili fedha ambazo zingetumika kwenye safari hizo za viongozi, zielekezwe katika shughuli nyingine za maendeleo ya nchi kama ambavyo tumeainisha baadhi yake.

Ni wazi kwamba kwenye safari hizo za kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam, kuna kulipwa posho za kulala, mafuta, lakini pia vipuri vya magari vinachakaa, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa matumizi ya fedha.

Lakini tunaamini kwamba, matumizi hayo yanaweza kubanwa iwapo viongozi wataona umuhimu wa kufanyia mikutano, makongamano na vikao kwenye makao makuu ya nchi ambayo yako Dodoma.

Kadhalika, kuna uwezekano wa kufanya mikutano mingine kwa njia ya mtandao kama ambavyo imekuwa ikifanyika ikiwa tahadhari ya kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19.

Tunatarajia kuona tabia hiyo inadhibitiwa, ikizingatiwa kuwa Spika Ndugai alilielekeza angalizo hilo kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye anaratibu shughuli za serikali za kila siku. Vinginevyo, uamuzi wa Dodoma kuwa makao makuu ya nchi na serikali hautakuwa na maana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mike Taseni

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Hii ndiyo maana ya Rais Samia, kutangazwa Hangaya*

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, ametangazwa kuwa chifu wa mkuu wa machifu wote nchini, akipewa cheo cha Hangaya. Ni jina jipya katika msamiati ila maana yake ni kuwa ni 'nyota inayong'ara,' mpangilio wa hisia ambao unaleta faraja.

Ukiangalia eneo au mkoa ambako tamasha hilo liliandaliwa, na mpangilio wa wahusika wake kuwa ni machifu wote nchini au watemi waandamizi kutoka makabila ya mikoa tofauti, unapata hisia kuwa siyo wazo la hivi karibuni. Ina maana kuwa ni shughuli iliyokuwa imepangwa mapema na siyo katika miezi hii michache ambako Rais Samia amekuwa madarakani. Inaelekea kuwa ilibidi wahusika wajipange upya, waangalie kama tamasha hilo linaweza kuendelea au hapana, wakaona inabidi liendelee.

Ni mwelekeo unaoshabihiana kwa undani na kauli mbiu ya Rais Samia, akitoa salamu yal jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupokea itikio kuwa 'kazi iendelee,' na kwa maana hiyo dhamira ya kuwa na umoja wa machifu nchini, na Rais kuwa mkuu wao, ni kazi iliyopangwa, ikabidi 'iendelee.' Suala hapa ni kama tathmini yake kisiasa na kitamaduni inabaki pale pale au imebidi ichukue mwelekeo tofauti, au tuseme kuinia hisia chanya za mpangilio tofauti, ukilinganisha na dhamira yake wakati wa awamu ya tano. Unaweza hata kujiuliza kama mwelekeo wa sasa kisiasa una nafasi ya umoja wa machifu, kitaifa.

Kutangazwa Haganya kwa Rais Samia kulikuwa na maana iliyotarajiwa au inayoeleweka kwa haraka, yaani kupata ridhaa nyingine au ya ziada ya uongozi wake, kwa kuinua hisia za utii kutoka eneo jingine ambako awali halikuwa sehemu ya kutolewa kwa ridhaa ya kuwa kiongozi wa nchi. Hata hivyo ni ridhaa ya heshima tu ambayo haibadili chochote kikatiba lakini inagusa mapana na marefu ya utii kwake kama kiongozi wa nchi kwa upande mmoja na kwa nafsi yake binafsi. Utii hasa si kwa nafasi tu ya yule ambaye kiapo cha utii kinatolewa kwake ila una eneo la ziada, yaani kwa nafsi yake pia kana mtu binafsi.

Kinachoonekana ni kuwa tamasha hilo liliandaliwa nyakati za awamu ya tano kwa dhamira ya kutoa ridhaa maalum ya utawala wa kiongozi mkuu wa wakati huo, iwe ni kukubalika kwa kiongozi mkuu kitaifa.

Inaelekea pia matayarisho yake yalikuwa yamefikia hatua kubwa, suala likiwa siyo tu kutambuliwa kwa kiongozi mkuu kama mkuu wa machifu, ila kuingiza dhana ya uongozi usiotofautiana na uchifu, ambao kimsingi hauna 'mihula ya uongozi. Baada ya awamu ya tano kukatika ikiwa nusu ya wakati wake wa kawaida, tamasha hilo ni kama kuokoa kinachowezekana bado.

Ina maana kuwa taifa kwenye tamasha ambalo tayari sura yake ilishabadilika, kutoka tamasha la kisiasa kuwa tamasha la kitamaduni, kwani Hangaya wa hivi sasa ana msingi wa kikatiba wa kuwapo madarakani ambao hauwezi kujitanua ukawa mithili ya uchifu, unaorithishwa baada ya kifo.

Ni heshima inayoendana na ngazi ya uongozi, huku ngazi hii ikiwa inatokana na mamlaka tofauti yenye mpangilio tofauti wa uwepo wake. Ila wakati tamasha hilo linapangwa, inaelekea ilitazamiwa kuwa maeneo hayo mawili yangeweza kuoanishwa, hivyo utawala wa kikatiba wenye mihula uinuliwe kuwa utawala wa jadi usio na hii mihula.

Matamasha ya kuoanisha ngazi ya kikatiba kuwa ngazi ya jadi yamekuwapo Afrika tangu uhuru, kwani Afrika iliachiwa mfumo wa Ulaya ni wa kikatiba ila walioingia madarakani kwa sehemu kubwa walikuwa katika jadi. Na licha ya vita ya muda mrefu kati ya jadi na dini, wengi bado wako katika jadi kutokana na kupeana maeneo, kati ya jadi na dini. Viongozi wa Afrika wamejitahidi kuheshimu dini.

Kwa maana hiyo tamasha la kumsikika Rais Samia kuwa Hangaya limeondoka katika dhamira yake ya awali ya kuinua utawala wa kikatiba uwe wa jadi, na badala yake jadi ikubaliane na utawala wa kikatiba ulipo.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
### WAKALA YA BARABARA TANZANIA

# SALAMU ZA PONGEZI



*Prof. Makame M. Mbarawa (Mb.) Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.*

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa **TANROADS,** tunakupongeza **Prof. Makame M. Mbarawa (Mb.)** kwa kuteuliwa na kuapishwa na **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**TANROADS** tunaamini kuteuliwa kwako ni ushahidi wa uwezo wako wa kutekeleza sera ambazo ni chachu katika kuleta maendeleo ya dhati kwa Taifa letu.

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA***

**TANROADS Makao Makuu**
**Ghorofa ya 1-3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue**
**S.L.P 11364 Dar Es Salaam**
**Baruapepe:Tanroadshq@tanroads.go.tz**

***www.tanroads.go.tz***

# Shule za CCM zafungwa kisa kukosa wanafunzi

**Na Shaban Njia,**KAHAMA

SHULE za sekondari nane kati ya 58 zinazomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi (TAPA) ya Chama Cha Mapinduzi nchini zimefungwa kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukosa wanafunzi.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo Taifa, Gilbert Kalima, huku 25 zikihitaji maboresho.

Kalima alikuwa akizungumza na viongozi wa CCM Mkoa wa Shinyanga baada ya kufanya ziara ya siku moja ya kikazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Aidha, alisema jumuiya ina jumla ya shule za sekondari 58 nchi nzima, huku shule hai zikiwa 50, shule nane zikiwa zimefungwa kwa kukosa wanafunzi na kuwa na miundombinu chakavu na shule 25 kati 58 zikiwa zinahitaji kufanyiwa maboresho.

Alisema kuwa wana kazi kubwa ya kuziboresha shule hizo ili kuhakikisha zinatoa elimu bora kwa wanafunzi waliopo na kuwataka viongozi wa jumuiya ambapo shule hizo zinapatika kufuatilia kwa undani matatizo ya shule hizo na kuzitafutia ufumbuzi wa pamoja.

"Wakati nateuliwa moja ya jukumu nililokabidhiwa lilikuwa kuhakikisha shule zote zinakuwa imara na kutoa elimu kama ilivyokusudiwa na ndio maana nimeanza kufanya ziara ya ufuatiliaji kujua hali halisi ya shule zetu zipo katika hali gani," alisema Kalima.

Awali akisoma taarifa ya wilaya, Katibu wa Jumuiya hiyo Wilaya ya Kahama, Regina Ndulu, alisema, Shule ya Sekondari Wigehe ina jumla ya wanafunzi 17, wa kiume saba na wakike 10, huku kidato cha pili kikiwa hakina wanafunzi kabisa.

Alisema kidato cha kwanza kina wanafunzi wanne, wakike watatu na wakiume mmoja, kidato cha tatu wakiwa wanafunzi watatu, wanafunzi wa kiume wawili na kike mmoja na kidato cha nne kikiwa na wanafunzi 10, wa kiume wanne na wakike sita.

Hata hivyo, alisema walimu waliopo shuleni hapo ni watano ambao wote ni wa kujitolea isipokuwa mwalimu mkuu. Walimu hao wa kujitolea ni wa kike mmoja na wa kiume wanne na kwamba shule hiyo inashindwa kujiendesha kwa kukosa wanafunzi na kusababisha kuanzisha mradi wa kuuza molamu kwa lengo la kuendesha shule.

Hata hivyo, alisema, kuwapo kwa mradi huo kumesababisha kuwapo kwa migogoro kati ya mwalimu mkuu na baadhi ya walimu wa shule hiyo ambapo kila mmoja amekuwa akikusanya fedha na kuziweka mfukoni badala ya kuziwasilisha kwa mhasibu wa shule.

Nae Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Revocatus Paschal, alisema alipoanza kazi Januari mwaka huu, alikuta shule hiyo ina jumla ya wanafunzi sita na kuchukua jukumu la kuongeza wanafunzi hadi kuchukua baadhi ya wanafunzi kutoka Sekondari ya Magufuli Chato mkoani Geita na kufikia 17.

Kuhusu mali za shule, alisema ameamua kuwasimamisha kazi walimu baada ya kutuhumiwa kuhujumu mali za shule kwa kuiba mageti, vifaa vya maabara, kupokea ada za wanafunzi kinyume cha utaratibu kwa madai wanajilipa mishahara.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akizungumza na washiriki waliohudhuria uzinduzi wa agenda ya mtoto njiti iliyodhaminiwa na Taasisi za Vodacom Tanzania Foundation kupitia Doris Mollel Foundation, jijini Dodoma. Kwa miaka mingi taasisi hiyo imekuwa ikisaidia kutatua changamoto za afya hapa nchini kwa kutumia teknolojia kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yapewa angalizo kuhusu selimundu

**Na Christina Mwakangale**

WITO umetolewa kwa jamii hususan walio kwenye mahusiano na wanaotarajia kuoana, kufanya vipimo kubaini iwapo wana magonjwa ambayo yanahusisha vinasaba ili kupunguza uwezo mkubwa kurithisha watoto wanaowatarajia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi zinazojishughulisha na Ugonjwa wa Selimundu Tanzania (TANSCDA), Dk. Deogratius Soka, amesema vipimo vya kitabibu, hutoa picha ya hali ya afya za wahusika ikiwamo dalili za ugonjwa wa selimundu.

Dk. Soka aliyasema hayo jana katika mahojiano ya moja ya kipindi cha makala ya afya katika televisheni, akizungumzia ugonjwa huo na kwamba nchini asilimia 15 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu.

"Hatufikirii kwamba kupima wakati wa kuoana ni kipindi kizuri sana, kwa sababu watu waliofikia hatua ya kwenda kwa shehe au kanisani kutaka kufunga ndoa, hatua ambayo huwezi kuirudisha nyuma.

"Hivyo vijana wapime kabla hawajaanza mahusiano, ili wajijue na ambao wana vinasaba wataweka lengo la kwamba mwenza nitakayempata asiwe na vinasaba hivyo. Kwa ambao tayari wamaeoana na wana vinasaba wote, hatushauri waachane.

"Wajue kwamba sisi tunaweza kupata mtoto mwenye selimundu na wakawahi kumpima mtoto itamuepusha mtoto na madhara yatokanayo na selimundu," alieleza bingwa huyo.

Dk. Soka alisema tatizo lililopo kwenye ugonjwa huo tofauti na mengine, kwa kuwa selimundu hukaa katika vinasaba hivyo ni kati ya maradhi ambayo yanarithiwa na kwamba sio ugonjwa wa unaoambukiza, na anayeugua maradhi hayo hurithi na kurithisha wengine uweze

"Ugonjwa huu hauwezi kumpata mtu asiye na selimundu hata akiongezewa damu na mtu mwenye selimundu sababu ni ugonjwa unaokaa kwenye vinasaba. Mtu mwenye selimundu damu yake yote ina selimundu."

Dk. Soka alisema tatizo kubwa kwa ambao wanaugua selimundu ni kuishiwa damu kila mara na kuhitajika kuongezwa, kutokana na chembechembe zao za damu kuishi kwa muda wa siku 10 HADUI 20, huku asiyeugua kawaida huishi siku 90 hadi 120.

Kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini, alisema duniani watoto 300,000 huzaliwa kila mwaka na ugonjwa wa selimundu, wakati 11,000 hadi 12,000 kila mwaka huzaliwa Tanzania ikishika nafasi ya nne na hadi sasa kuna watoto 300,000 na kwamba selimundu huchangia vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano kwa asilimia 6.7.

"India, Nigeria, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) inafuatia Tanzania katika idadi ya wanaougua selimundu. Asilimia 15 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu," alisema Dk. Soka.

# TCCIA yawaahidi makubwa w/biashara

**Na Mwandishi Wetu**

CHEMBA ya Wafanyabiashara wenye Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) imepata mkurugenzi mtendaji wake mpya ambaye pamoja na mambo mengine, ameahidi kuifanyia marekebisho sambamba na kuwaleta pamoja wadau wote wa sekta hizo.

Akizungumza baada ya kutambulishwa kwa wafanyakazi na Rais wa Chemba hiyo, Paul Koyi, Judith Karangi, ameihakikishia bodi ya wakurugenzi na wafanyakazi kuwa atafanya kazi kwa bidii na weledi mkubwa ikiwamo kurejesha imani kwa wafanyabiashara wote nchini."Kwa dhati kabisa ninapenda kuwahakikishia kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa ufanisi ili sisi kama taasisi muhimu ya kuwaunganisha na kuwasaidia wafanyabiashara tunatekeleza wajibu wetu kwa weledi," alisema Karangi.

Pia alizungumzia nafasi ya TCCIA katika kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025 na kuahidi kufanya kazi kwa karibu na taasisi za serikali.

"Nina uhakika tupo vizuri kwa kushirikiana na wadau wote tutaifikisha Tanzania mahali pazuri," alisema na kuomba ushirikiano kutoka kwa wafanyakazi, menejimenti, bodi ya wakurugenzi na wadau wengine wote.

Awali, akimtambulisha, Koyi alielezea imani kubwa aliyonayo pamoja na bodi ya wakurugenzi kwa mkurugenzi mtendaji mpya kwani ataipaisha TCCIA kutoka ilipo sasa na kusonga mbele zaidi.

"Imani niliyonayo na bodi pia kwa mtendaji wetu mpya ni kubwa na matumaini yetu yanakwenda mbali zaidi kuona kwamba kwa uzoefu alionao utakuwa chachu ya kufikia malengo ambayo taasisi imejiwekea," alisema Koyi. Aidha, Rais huyo wa TCCIA aliwahimiza wafanyakazi wa taasisi hiyo kumpa ushirikiano mkurugenzi mtendaji huyo na kueleza kuwa mafanikio ya taasisi hiyo yatategemeana na umoja na ushirikiano kwenye utendaji wa kazi.


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(COMMERCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

COMMERCIAL CASE NO. 68 OF 2020

R & K TRUCKING CO. LTD.............................................PLAINTIFF
VERSUS
SABIHI RASHID NOKOLAGE.............................................1ST DEFENDANT

JOE OCEAN CLEARING AND FORWARDING
COMPANY LIMITED.............................................2ND DEFENDANT

SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION

TO:
SABIHI RASHID NOKOLAGE,
MBAGALA,
P.O.BOX 46343, DAR ES SALAAM.
MOBILE: 0688 258059

TAKE NOTICE that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars set out in the plaint filed in this court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication.

You are directed to collect copies of the summons and plaint from the Court's Registry, P.O.Box 12533, Dar es salaam. You are ordered to file your written statement of defence within twenty one (21) days of publication of this notice. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 15th & 18th day of October, 2021 at 10:00 am when this case will be heard.

TAKE FURTHER NOTICE THAT should you default to file your written statement of defence and/or enter appearance as herein provided, the suit will proceed and a decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 8th day of September, 2021.

DEPUTY REGISTRAR

164573022

HABARI KITAIFA

# Mradi kusaidia watoto 700 kutoka familia duni

**Na Francis Godwin,** IRINGA

VIJANA na watoto wanaotoka katika familia duni zaidi ya 700 katika vijiji 16 vya kata za Luhunga, Mdabulo na Ihanu, Wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa wanatarajiwa kusaidiwa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), kuondokana na tatizo la ugumu wa maisha.

Mradi huo pia umesaidia watoto yatima 51 baadhi yao wazazi wao wamepoteza maisha kwa janga la Ukimwi, kwa kuanzishiwa makazi maalum katika Kijiji cha Igoda, Kata ya Luhunga, Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa kwa ajili ya kusaidia mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidiwa kupata elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

Akitoa taarifa hiyo jana kwenye kikao kazi cha mradi huo wa Youth Agency Mufindi (YAM), Meneja wa mradi, Danford Mkumba, alisema mradi huo utasaidia pia kutoa mafunzo yatakayowezesha vijana hao kujikwamua kiuchumi.

Alisema watoto hao wameendelea kupata malezi bora ikiwamo elimu na kuwa pamoja na wenzao kupitia mradi wa YAM vijana na watoto wanaotoka katika familia duni 770 wanatarajia kusaidia na mradi huo kupata elimu ikiwamo ya ufundi wa uselemara kwa watoto wa kike pamoja na kuwapatia vifaa vya kuanzishia viwanda vyao.

Alisema mradi huo upo chini ya Foxes Community and Wildlife Conservation Trust (FCWCT), unafadhiliwa na Deaconess Foundation ya nchini Finland na kwa Wilaya ya Mufindi mradi huo unatekelezwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Hata hivyo, alisema mradi huo umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka huu na tayari umekwisha andaa wajumbe 160 kutoka vijiji 16 vya kata tatu ikiwamo Ihanu, Luhunga na Mdabulo zote za wilayani Mufindi kuwa mbali ya wajumbe hao kutakuwa na timu ya mradi kutoka Tanzania na Finland, timu ya uwezeshaji kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, viongozi wa vijiji vyote ambavyo mradi utatekelezwa pamoja na halmashauri zao.

Alisema malengo ya mradi huo ni kuwahusisha vijana wenye ulemavu katika mfumo rasmi wa ajira na ujasiriamali, kuwezesha vijana walio katika mazingiramagumu kujitegemea na kujisimamia wenyewe kutumia fursa mbalimbali zilizopo kwenye maeneo yao.

Pia, kuwaondoa vijana katika tabia zenye athari kwenye maisha yao, kupunguza au kuondoa wimbi la vijana kuhamia mijini kufanya kazi za ndani pia kuleta usawa wa kijinsia katika kuibua na kutumia fursa zilizopo katika jamii.

Alisema mradi huo utaendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana, elimu ya saikolojia, mafunzo maalumu kwa mabinti, mafunzo kwa jamii kuhusu kuwatunza watoto wenye ulemavu na nama bora ya kutumia fursa zinazozunguka pamoja na mafunzo ya kilimo cha mazao ya chakula, kilimo cha miti ya mbao na nguzo za umeme na shughuli nyingine nyingi.

Mwenyekiti wa chama cha watoa huduma za kisaikolojia Tanzania, Dk. Heriel Mfangavo, alisema kutokana na ukubwa wa tatizo Halmashauri ya Mufindi kwa kushirikiana na mdau Fox chini ya ufadhili wa Finland wamekuja na mradi wa YAM ili kusaidia jamii Wilaya ya Mufindi.



Mwalimu wa Chuo cha Utalii cha Udzungwa Mountain College Trust (UMCTO) cha mjini Moshi, Edgardo Welelo (kulia), akitoa maelezo kwa wanafunzi wa chuo hicho wakiwa katika ziara ya mafunzo eneo la Ziwa Momella, katika hifadhi ya taifa ya Arusha National Park **(ANAPA) jana. PICHA: JAMES LANKA**

## Wakerwa adhabu ndogo kwa wafujaji mali za umma

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WAFANYABIASHARA mkoani hapa wamesema wanakatishwa tamaa ya kuendelea kulipa kodi kwa serikali kutokana na adhabu ndogo zinazotolewa na mahakama kwa watendaji wa serikali wanaopatikana na hatia ya kufuja fedha za umma, ambazo zinatokana na kodi zinazotolewa na wananchi.

Walitoa malalamiko kwa Mkurugenzi wa Elimu kwa mlipakodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo.

James Moses, akiuliza swali katika mkutano huo uliofanyika mjini Tunduma, alisema adhabu hizo zinakatisha tamaa walipa kodi.

Alisema kitendo cha mahakama kutoa adhabu ndogo kwa watu waliopatikana na hatia ya kufuja fedha za umma kinawakatisha tamaa wafanyabiashara ambao wamekuwa waaminifu kulipa kodi za serikali kwa lengo la kusaidia maendeleo ya nchi.

"Unakuta mtumishi wa serikali amefuja fedha za walipa kodi na akipelekwa mahakamani unasikia katozwa faini ndogo ukilinganisha na fedha alizotafuna...hali hii inatukatisha tamaa sana sisi walipa kodi" alisema Moses.

Hata hivyo, alishauri watumishi wote wanaokutwa na hatia za makosa ya ufujaji wa fedha za walipa kodi wafilisiwe na TRA ipewe uwezo wa kisheria wa kuwanyima fursa ya kufanyabiashara yeyote.

Akijibu maswali ya wafanyabiashara hao, Kayombo alisema malalamiko yao ni ya msingi kwa kuwa walipakodi na wananchi wanahaki ya kuhoji matumizi ya fedha zao.

Aidha, Kayombo aliwataka wafanyabiashara katika mji wa Tunduma kuacha kutumia njia za panya kuingiza bidhaa za magendo nchini kwa kuwa ni hatari kwa usalama wa nchi.

Alisema kuna baadhi ya bidhaa kutoka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) hazitozwi kodi yeyote kikubwa bidhaa hizo ziwe na taarifa sahihi za uthibitisho kuwa zinatoka miongoni mwa nchi za jumuiya hiyo.

# Kunenge aagiza kasi ujenzi wa daraja la Mbuchi

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameielekeza Kampuni ya Alpha Logistick inayojenga daraja la Mbuchi kuharakisha ujenzi huo kuondoa adha wanayokabiliana nayo wananchi wanaovuka eneo hilo kwa sasa wanatumia mitumbwi.

Kunenge ametoa agizo hilo alipokuwa kwenye ziara ya kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani ambayo ilikuwa ikikagua miradi ya maendeleo ukiwamo ujenzi wa daraja hilo.

Alisema kukamilika kwa daraja hilo kutawawezesha wananchi kusafirisha bidhaa zao kwa wakati kutoka vijiji vya Mbwela kwenda Muhoro na maeneo mengine ya wilaya za Rufiji na Kibiti.

"Naishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya maendeleo katika mkoa wetu, miradi ambayo ni suluhisho la kuondoa kero za wananchi, kazi yetu viongozi ni usimamizi ikamilike kwa wakati," alisema.

Kaimu Mhandisi mkazi wa mradi, Mtani Silasi, alisema mradi huo ambao utatekelezwa katika wilaya za Rufiji na Kibiti ni wa miezi 12 na unatarajia kukamilika mapema mwaka 2022 kwa gharama ya Sh. bilioni 6.1.

Alisema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 31, na kwamba kuharibika kwa mitambo mara kwa mara kutokana na mawe na magogo yaliyowekwa katika ujenzi wa awali ni moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo.

Maulid Omari, mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Mbwera, alisema ujenzi wa daraja hilo utawaondolea kero ya gharama za mitumbwi na boti wanazotumia kuvuka kwa sasa.

Omari alisema bidhaa za biashara wanazosafirisha zinashindwa kufika kwa wakati sokoni, kutokana na wakati mwingine kutumia zaidi ya saa sita wakisubiri maji yajae ndipo boti wanazotumia ziwavushe hadi Muhoro.

Alisema mbali ya bidhaa za biashara, pia wanalazimika kutembea kilometa nane hadi kumi kwenda kwenye shughuli za kilimo kutokana na kukosekana daraja na pia wananchi wengi kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za kulipia boti za kuwavusha kutoka Mbwera.

Hadija Selemani, mkazi wa Mbuchi alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za ujenzi wa daraja hilo kuokoa wananchi ambao wengi wao hususani wanawake wamekuwa wakikumbana na kero wakihitaji kuwahishwa katika kituo cha afya kilichopo Mbwera.

Daraja hilo litawasaidia wananchi wa vijiji zaidi ya saba ambao wanafanya biashara za nazi na samaki kuzifikisha mapema sokoni

# Bil. 27/- kutatua kero ya madarasa Geita

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SERIKALI kuu imetoa Sh. bilioni 27 kutatua kero ya uhaba wa vyumba vya madarasa mkoani Geita.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Staki Senyamule, alipokuwa akizindua Shule ya Sekodari binafisi Royal Famili iliyopo katika Mtaa wa Magogo Mjini Geita.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo kwa Mkoa wa Geita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya vyumba vya madarasa, huku akisema mkoa huo unakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 13,000.

Senyamule alisema licha ya fedha hiyo kutolewa mkoani humo, bado unahitaji fedha zaidi ili kuondokana kabisa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Mhandis Lazaro Jiyunga, alisema lengo la shule hiyo ni kuhakikisha wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza na kuhitimu kidato cha nne wanafaulu kwa madaraja ya kwanza, pili na tatu, hivyo kuwa kielelezo katika jamii.

Sheila Ramadhan ambaye ni mzazi, alisema kuna utofauti mkubwa katika ufundishaji kwa walimu wa shule binafsi na za serikali, hivyo kuiomba serikali kuweka motisha kwa walimu wa shule za serikali, hatua ambayo itasaidia wanafunzi kufanya vizuri.



Mwanaidi Abdalah, Mkazi wa Kata ya Kwagunda wilayani Korogwe mkoani Tanga, akifungua maji jana ikiwa ni Uzinduzi wa Mradi wa Maji uliojengwa na Shirika la World Vision Tanzania ( kushoto) ni Mkuu wa Wilaya hiyo Basila Mwanukuzi. **PICHA BONIFACE GIDEON**

# TRA, wadau wanolewa mabadiliko sheria za kodi

**Na Mwandishi wetu,** SIMIYU

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) inaendelea kutoa elimu ya mabadiliko ya sheria za kodi ya mwaka 2021 kwa watumishi wa mamlaka hiyo, wadau na walipakodi katika mikoa mbalimbali.

Akizungumza na watumishi, wadau na walipakodi hao katika mikoa ya Simiyu na Mara mwishoni mwa wiki, Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka TRA Makao Makuu Dar es Salaam, Zakeo Kowero, alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwa na uelewa mmoja kwa watumishi wa TRA na kwa upande wa walipakodi na wadau ni kuwafahamisha mabadiliko yaliyotokea ili kuongeza uhiari wa ulipaji kodi.

"Tumeamua kuzunguka kutoa elimu hii ya mabadiliko ya sheria za kodi yaliyofanywa na serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 ili kuhakikisha watumishi tunakuwa na lugha moja wakati tunawahudumia wateja wetu na kwa upande wa wadau na walipakodi ni kuwafahamisha kuhusu mabadiliko yaliyotokea," alisema Kowero.

Moja ya mabadiliko yaliyotokea ni kuongeza idadi ya waajiriwa kwenye Kodi ya kuendeleza Mafunzo ya Ufundi Stadi (SDL) kutoka wafanyakazi wanne hadi 10, lakini uwasilishaji wa ritani utaendelea kama kawaida bila kujali idadi ya watumishi.

Eneo lingine lililofanyiwa mabadiliko katika kodi hiyo ya uendelezaji mafunzo ya ufundi stadi ni la taasisi za kidini ambapo zimesamehewa kulipa kodi kwenye huduma za afya ya umma.

"Lengo la kuongeza idadi ya waajiriwa ni kuwapunguzia mzigo waajiri wadogo ili kukuza mitaji yao na dhumuni la kutoa msamaha kwenye taasisi za dini ni kuzipa unafuu katika kutoa huduma kwa jamii," alibainisha Kowero.

Akizungumzia mabadiliko yaliyofanyika katika kodi ya majengo, ofisa huyo alisema viwango vimeongezeka kwenye nyumba za kawaida katika majiji, manispaa na halmashauri za miji kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 12,000 kwa mwaka.

Kwa upande wa kila sakafu ya nyumba za ghorofa katika majiji, manispaa, halmashauri za miji, kodi imeongezeka kutoka Sh. 50,000 hadi Sh. 60,000 kwa mwaka na kwa nyumba za ghorofa zilizoko katika halmashauri za wilaya, kodi imeongezeka kutoka Sh. 20,000 hadi Sh. 60,000 kwa jengo zima kwa mwaka.

"Hata hivyo, serikali imebadilisha njia ya utozaji kodi hii ambapo kwa sasa kodi ya majengo inalipwa kupitia njia ya ununuzi wa umeme wa LUKU kwa kukata Sh. 1,000 kwa mwezi kwa nyumba za kawaida na Sh. 5,000 kwa mwezi kwa nyumba za ghorofa," alisema Kowero.

Kwenye Sheria ya Usajili wa Vyombo vya Moto, serikali imepunguza kodi ya usajili wa namba binafsi kutoka Sh. milioni 10 hadi Sh. milioni tano na usajili huo utadumu kwa miaka mitatu.

Ofisa huyo alisema lengo la mabadiliko hayo ni kuwavutia watu kusajili vyombo vyao vya moto na hivyo kuongeza mapato ya serikali.

Alisema mabadiliko mengine yamefanyika kwenye Sheria ya Ushuru wa Stempu, akitolea mfano kwamba ushuru wa stempu katika nyaraka mbalimbali umeongezeka kutoka Sh. 500 hadi Sh. 2,000.

Danieli Singiri, mmoja wa viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika wa mkoani Simiyu waliohudhuria semina ya mabadiliko ya sheria mkoani humo, alisema amefurahishwa na elimu hiyo na ameiomba serikali kuangalia kifungu kipya cha Kodi ya Zuio ya asilimia mbili iliyowekwa kwenye mazao ya kilimo kwa kuwa anaona kitawaumiza wakulima.

"Tumefurahi kwa kutupatia elimu hii muhimu lakini tunaiomba serikali iangalie Kodi ya Zuio ya asilimia mbili kwenye mazao ya kilimo kwani itawadidimiza wakulima kwa sababu watapokea fedha pungufu japokuwa lengo la kodi hii ni zuri na imelenga kuongeza mapato ya serikali. Ninashauri itafutwe njia nyingine tofauti na hii," alisema Singiri.

Elimu ya mabadiliko ya sheria za kodi imekwishatolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Kwa sasa elimu hiyo inaendelea kutolewa katika mikoa ya Simiyu, Mara, Mwanza, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

# Jamii yaonyeshwa fursa utalii Iringa

**Na Christina Haule,** IRINGA

JAMII imetakiwa kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini, likiwamo eneo la Kikongoma lenye historia ya mwanamama jasiri mkoani Iringa.

Mwanamke huyo aliona bora kujiua kuliko kuchukuliwa na maadui au kutaja siri za mwanae Chifu Mkwawa wakati wa mapigano na Wajerumani kweye miaka ya 1880.

Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na kundi la wanahabari wanawake 31 waliotembelea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kwa lengo la kutangaza na kuhamasisha utalii na uwekezaji nchini.

Alisema mwanamama huyo ambaye ni mama yake Chifu Mkwawa aliamua kujitumbukiza kwenye maji yaliyozungukwa na jiwe, huku kukiwa na tundu dogo la jiwe na kufariki dunia ili kuzuia asitekwe na maadui waliomtaka kutoa siri za Mkwawa.

"Historia hiyo imebeba ujasiri mkubwa kwa wamama, sababu mwanamke huyo alionyesha ujasiri na thamani ya mwanamke kwa kuamua kutoa roho yake kuliko kumwangamiza mwanawe kwa kutoa siri zake ... ninyi kama wanahabari wanawake na jamii kwa ujumla mnayo nafasi ya kufika na kujifunza," alisema.

Ngwada alisema Iringa ni mkoa wa kishujaa kwa sababu ya historia ya Chifu Mkwawa, ambaye alipigana vita kubwa kwa kutumia silaha za jadi na wenzake kwa kutumia silaha za moto, lakini yeye Mkwawa aliwashinda ambapo historia hiyo kubwa ipo makumbusho ya Karenga.

# Tamasha kutangaza vivutio utalii Mkuranga

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, inatarajia kufanya tamasha kubwa la kuvitangaza vivutio vya utalii Oktoba 2, mwaka.

Hayo yalibainishwa na mkuu wa Wilaya hiyo, Khadija Ally, katika kikao cha cha Baraza la madiwani, na kwamba Wilaya inamuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuutangaza utalii uliopo.

Alisema Mkuranga kuna utalii wa fukwe za bahati na wanyama.

" Hili tamasha likifanyika watu watajua utalii na vivutio vilivyopo katika Wilaya yetu na pesa zitakazokuwa zinapatikana kupitia utalii huo, zitaongeza mapato ya halmashauri," alisema na kuongeza kuwa maamuzi ya kutangaza vivutio vilivyopo Mkuranga ni juhudi za kumunga mkono,Rais Samia katika kuutangaza utalii kitaifa na kimataifa.

Alisema katika tukio hilo la kihistoria wamepanga pia kuwaalika wadau mbalimbali wa sekta ya utalii, huku, wakiongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro.

Aliwataka madiwani kushirikiana na watendaji kata wao kwa kuibua fursa mbalimbali za utalii kwenye maeneo yao kisha kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mwantumu Mgonja, aandae utaratibu juu ya kuwapo vivutio vya utali.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 14, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Ndivyo unyanyasaji unavyotisha japo upo mkakati wa MTAKUWA



Ukurasa 12

Fasihi inapotoa mwelekeo mpya kutibu changamoto za kielimu



Ukurasa 13

Angalia, 'shoti kati', kutojua haki kunavyokutumbukiza kwa matapeli

ELIMU

NA GWAMAKA ALIPIPI

ATHARI DAWA KULEVYA

# Mtaala sasa waja mafunzo kuanzia msingi hadi chuo

KATIKA kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya, Tanzania inajipanga kufundisha wanafunzi athari za dawa hizo kuanzia shule za msingi hadi ngazi za juu.

Ni jukumu linalofanywa na Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), ambayo inashughulikia maandalizi ya mtaala utakaoelimisha jamii kuhusu madhara ya dawa hizo.

Aidha, wanafunzi wa darasa la tatu wataanza kusoma somo la dawa za kulevya na kulifanyia mtihani, anasema Kamishna wa Kinga na Tiba wa DCEA, Dk. Peter Mfisi, katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam.

Anaongeza: "Tunaamini asilimia 90 hadi 99 ya Watanzania wanapitia elimu ya msingi, sekondari na kuendelea. Tunaamini tukiweka somo hilo kwenye mtaala wa elimu asilimia 99 ya Watanzania itakuwa imefikiwa na ujumbe wa dawa za kulevya".

Anabainisha kuwa hata kwa wanaotumia watafahamu madhara na kuongeza kwamba majadiliano yanaendelea na taasisi ya mitaala.

Anasema hata hivyo likiwa somo linalojitegemea litaongeza mzigo wa masomo kwa wanafunzi, hivyo watalipachika katika moja ya somo, lakini kwenye mitihani kutawapo na maswali yanayohusu dawa za kulevya.

Kwa sasa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inahitaji somo la rushwa liwepo kwa mtaala, ili kumpunguzia mzigo wa masomo mwanafunzi wa shule ya msingi kuna uwezekano kukawekwa somo moja litakalokuwa likifundisha masuala yote, lengo kuu ni watoto wote wanaopita katika mfumo wa elimu wawe na uelewa na madhara ya dawa hizo, anasema Dk.Mfisi.

### MAJUKUMU YA DCEA

Dokta Mfisi anaeleza kuwa ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa 2017, kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

"Huko nyuma kulikuwa na tume ya kudhibiti dawa za kulevya, ambayo iliratibu na kusimamia mapambano ya dawa za kulevya, ilikuwa haiwezi kukamata, kushikilia wala kuhukumu". Anasema Dk. Mfisi na kuongeza:

"Ilikuwa ikitegemea vyombo vingine vya ulinzi na usalama, kama vile polisi. Lakini DCEA ina mamlaka yote inapeleleza, inakamata, kupekua , kushikilia mali, pamoja na kuendesha kesi mahakamani."

Anaongeza kuwa inafanya kazi ya kupunguza uingiaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa kutumia divisheni ya intelijensia yenye kazi ya kutafuta taarifa za wauzaji wa dawa za kulevya, kujua mienendo yao.

Anaeleza kuwa divisheni hiyo ikishapata taarifa inazitoa kwa divisheni ya operesheni inayokamata wanaojihusisha na dawa za kulevya na kuwapeleka mahakamani, ambako kuna divisheni ya sheria " anasema Dk. Mfisi.



Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Dk. Peter Mfisi akizungumzia athari za matumizi ya dawa za kulevya. **PICHA: GWAMAKA ALIPIPI**

Anasema eneo jingine ni kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya nchini na kwamba DCEA inatoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya dawa hizo.

"Jamii kubwa haijui madhara ya matumizi ya dawa hizo, wengi wanadanganyana, wengine wanajua ukiuza utakuwa tajiri, ukitumia dawa utalima sana, kama ni mwanamuziki utaimba sana na kucheza hutachoka. Lakini hawasemi ukitumia utaathirika". Anaonya.

Anataja nguzo ya tatu ni kupunguza madhara yanayotokana na matumizi akiongeza kuwa DCEA inakuwa na jukumu la kutoa elimu kwa watumiaji wa dawa, ili kuziacha kwa sababu ya kuwa hatarini kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Mbali na hilo anasema wanasimamia vituo 11 vya kutolea tiba kwa waraibu, ambao hadi kufikia Desemba mwaka jana walikuwa wamesajiliwa ni 10,565 wanaopewa dawa ya methadone katika vituo vitatu vilivyoko Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Pwani, Bagamoyo, Arusha, Dodoma na Tanga.

Dokta Mfisi anakumbusha kuwa wauza dawa hizo hawana mipaka kwamba mfanyabiashara anakuwa na mtandao katika nchi mbalimbali, hivyo ili kuwadhibiti DCEA inashirikana na mataifa mbalimbali yanayojihusisha na mapambano na dawa za kulevya.

"Kwa mfano anaweza kutoka Tanzania anasafiri kwenda nje, tukamhisi amebeba dawa, lakini taarifa zilichelewa kutufikia, wakati tunamfuatilia ameshaingia kwenye ndege labda anakwenda jijini Hong Kong , hivyo tunawasiliana na wenzetu wa Hong Kong kumdhibiti".

### WALIOFUNGWA NJE

Kamishna Mfisi, anasema mwaka 2018, Watanzania waliokuwa wamefungwa ng'ambo kutokana na kujihusisha na usafirishaji wa dawa za kulevya walikuwa zaidi ya 1,000.

Anafafanua kuwa kuna wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya waliokuwa wanasumbua na wengi wamekamatwa na kuhukumiwa, wengine kesi zao zinaendelea.

INAENDELEA UK.13

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Fasihi inapotoa mwelekeo mpya kutibu changamoto za kielimu

SHULE za msingi za Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, zina mengi ya kuigwa, mojawapo ni namna zinavyoipa umuhimu fasihi katika kufikisha ujumbe wa kupambana na changamoto za kielimu.

Hilo linafanikishwa kwa kutumia klabu ya fahisi, ambayo japo haijapewa kipaumbele kama zilivyo nyingine mfano za kupinga rushwa, michezo na ulinzi wa mabinti, inatajwa kuwa ina umuhimu wa kipekee kufanikisha lengo la kusaidia kukuza elimu.

Ofisa Elimu Msingi wa wilaya hiyo, Mwinoki Chacha, akiwa kwenye tamasha la kutoa tuzo za fahisi ya Kiswahili lililofanyika hivi karibuni Kisarawe, anaagiza shule za msingi za eneo hilo kuwa na klabu za fasihi.

Anaelekeza zitumiwe kuwawaandaa vijana kutunga hadithi zinazoelezea matatizo yao kuanzia utoro na mimba za utotoni na vishawishi vya madereva wa bodaboda kwa wanafunzi.

Mengine anayotaka yafanyiwe kazi ni pamoja na matatizo ya kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu, ili kuhakikisha wanafunzi wanaanza darasa la kwanza hadi wanahitimu elimu yao bila kukutana na mambo yatayowakwamisha njiani.

"Kila shule ya msingi iwe na klabu za fahisi, ili ziwasaidie wanafunzi kupenda kusoma na kujisomea, pia kuepuka vishawishi vinavyoweza kuwakwamisha kielimu," anasema Chacha.

Ofisa elimu huyo anasema hayo baada ya kushuhudia wanafunzi watatu wa shule za Msingi Chanzige A na B pamoja na Sanza wakiibuka kidedea kwenye mashindano ya kutunga hadithi katika mashindano ya fasihi ya Kiswahili.

Mashindano hayo yaliyoandaliwa na asasi ya Tanzania Fasihi Fund (TAFF), kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi kutunga hadithi zinazoweza kusaidia kudhibiti utoro.

Katika mashindano hayo, Ummy Werema, anayesoma darasa la sita Chanzige B, aliibuka mshindi, wakati Ng'orongo Elia wa darasa la sita Chanzinge A, alikuwa namba mbili.

Nafasi ya tatu ilichukuliwa na Denis Mwanga wa darasa la tano, akitokea shule ya Sanza.

Katika mashindano hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Wilaya ya Kisarawe, Patrick Gwivaha, anashauri mashindano hayo yaboreshwe, ili yawe na washiriki wengi, baada ya kuonyesha kuwa yana umuhimu mkubwa.



Mkurugenzi wa TAFF, Hussein Wamaywa akizungumza kwenye tamasha la utoaji tuzo. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Patrick Gwivaha. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Muda wa mashindano na tamasha la utoaji wa tuzo vimekuwa vifupi, washiriki wamekuwa wachache, pamoja na hayo tumeona jinsi watoto walivyo na uwezo wa kutunga hadithi.

"Muda wa mashindano na tamasha la utoaji wa tuzo vimekuwa vifupi, washiriki wamekuwa wachache, pamoja na hayo tumeona jinsi watoto walivyo na uwezo wa kutunga hadithi," anasema Gwivaha.

Anasema, njia inayoweza kusaidia kuboresha mashindano na utoaji wa tuzo ni kuwa na maandalizi ya kutosha, ili kusaidia zaidi wanafunzi kupenda elimu na kuepuka vishawishi vinavyoweza kuwakamisha maendeleo yao ya elimu.

## MSHINDI ANENA

Ummy Werema, anasema tuzo hiyo imempa hamasa ya kuandaa hadithi nyingi zaidi za kusaidia wanafunzi wenzake kuwa makini na vishawishi vinavyoweza kuwaharibia maendeleo yao kwenye elimu.

Mwanafunzi huyo anasema, alitunga hadithi aliyoipa jina la Zawadi na Mashaka, ambayo ilizungumzia watu hao wawili, Mshaka akiwa hapendi shule, lakini zawadi akiwa makini darasani.

" Mashaka alikuwa hapendi shule kwa sababu alitegemea mali za baba yake, lakini matokeo yake mali ziliisha na kujikuta akiwa hana kitu.Lakini Zawadi alisoma akahitimu na kufanya kazi," anasema Ummy.



Ofisa Elimu Msingi Mwinoki Chacha, ambaye ameziagiza shule zote wilayani mwake kuwa na klabu za fasihi. **PICHA: SABATO KASIKA**

Anaongeza kuwa hadithi yake imegusa wanafunzi wenzake, walimu na wazazi, na kwamba kila mmoja atafanya sehemu yake, ili kuhakikisha elimu inapewa kipaumbele zaidi kuliko mambo mengine.

Mkurugenzi wa TAFF Hussein Wamaywa, anasema mashindano yalifanyika Septemba mwaka 2020, lakini wakashindwa kutoa tuzo kutokana na janga la corona.

"Tumekaa mwaka mmoja hadi wiki iliyopita tulipofanya tamasha la kutoa tuzo hizo kwa washindi kuanzia wa shule za msingi hadi sekondari, ambao wote wamekadhiwa tuzo zao," anasema wamaywa.

Wamaywa anafafanua kuwa walianzisha mashindano hayo wilayani Kisarawe kwa lengo la kuunga mkono juhudi za aliyekuwa mkuu wa wilaya hiyo Jokate Mwegelo za kutokomeza ziro.

"Kwa upande wa sekondari, mshindi wa kwanza alikuwa ni Johnson Winga wa kidato cha nne katika Shule ya Gongoni, mshindi wa pili ni Hamis Hamis wa kidato cha sita kutoka shule ya Maneromango," anasema na wa tatu ni Tariq Yahaya wa kidato cha nne katika shule ya Gongoni.

"Watu wazima na hata wanafunzi wamekuwa ni wazito katika usomaji wa vitabu, lakini tunaamini kwamba kupitia hadithi fupi zilizomo kwenye vitabu tunavyoandaa zinaweza kuwabadilisha," anasema.

## VITABU KIBAO

Anasema, mbali na kutoa tuzo kwa washindi, TAFF kwa kushirikiana na wadau wengine, wamekabidhi vitabu 270, kwenye tamasha hilo ambavyo vitatumiwa na wanafunzi kujifunza mambo mbalimbali.

Mkurugenzi huyo anawataja baadhi ya wadau hao kuwa ni Reading Marathon, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA).

Vitabu tulivyotoa ni vya hadithi za watoto na watu wazima. Ni matumaini yetu kwamba vitakuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha jamii kupenda kusoma, pia kusaidia wanafunzi kupenda elimu.

"Lengo letu jingine ni kutaka kurejesha ari ya kusoma, pia kuwafanya watunzi wa hadithi kutunga vitu ambavyo vinaweza kuhamasisha jamii kubadilika na kupenda mambo mema badala kuegemea kwenye utunzi wa hadithi za mapenzi pekee."

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Angalia, 'shoti kati', kutojua haki kunavyokutumbukiza kwa matapeli

KILA Mtanzania anazo haki anazostahili ,mfano kwa kuzaliwa anastahili kuishi, kulindwa na kutoa maoni , yote ni kwa mujibu wa katiba, sheria, kanuni na taratibu za kitaifa na kimataifa.

Haki za binadamu zinasisitizwa ndani ya Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (UDHR) la mwaka 1948, linatoa fursa kwa kila mtu kupata haki anazostahili, bila kizuizi chochote.

Haki hizo zinagusa masuala ya kijamii ajira, kupanda cheo, kiuchumi kufanyabiashara, kuwekeza , kisiasa kama kuwa na chama, kugombea uongozi, kushiriki uchaguzi na masuala kama hayo.

Hivyo, ni muhimu kila mmoja kuzijua haki hizo na nyingine muhimu, kutumia sheria na taratibu kuzipata na kutimiza wajibu wake katika kuwapa haki wanazostahili wengine ili, kujenga jamii yenye utulivu, ustaarabu na ustawi wa kimaendeleo kikatiba na kwa mujibu wa UDHR.

Watumishi wa umma, wafanyakazi wa sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ni makundi muhimu katika ujenzi wa taifa na maendeleo yake. Ndiyo ambao kwa juhudi zao, wanachangia ustawi bora wa maendeleo ya nchi yao, kwa kutoa na kupokea haki.

Hivyo basi, makundi haya yanayo fursa ya kupata haki zao kwa mujibu wa sheria, bila mkwamo wa aina yoyote pale wanapohitaji kupata haki hizo hasa katika suala la kuhudumiwa na mamlaka zilizopewa jukumu hilo na serikali, ambayo inapata mamlaka kutoka kwa wananchi.

Kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hapa nchini, baadhi ya Watanzania wasio waaminifu wanatumia sayansi na teknolojia yake katika matumizi yasiyo sahihi ikiwapo suala la utapeli wa mitandaoni.



Wananchi wakizijua haki zao watatoa taarifa za matapeli polisi badala ya kuwatumia fedha wanazotaka, ili kuwapa huduma. **PICHA: MTANDAO**

Baadhi ya wahanga wa utapeli wa mitandaoni ni pamoja na watumishi wa umma na wananchi hasa wasiofahamu mambo yanavyokwenda hasa wakazi wa vijijini na pembezoni.

Matapeli wamekuwa wakituma ujumbe mfupi wa maneno (SMS) na wakati mwingine kuwapigia simu watumishi wa umma na wananchi wakijitambulisha kama maofisa wa serikali wakiwalaghai watume fedha, ili waweze kusaidiwa katika masuala mbalimbali.

Hayo ni pamoja na uhamisho, kuteuliwa katika nyadhifa mbalimbali, kulipwa malimbikizo ya madai yao, kupanda vyeo au madaraja, kulipwa mafao ya kustaafu, kupata ajira mpya na hata kwenda kuongeza ujuzi.

Wakati mwingine kutokana na kiu na uharaka wa kupata haki zao, baadhi ya watumishi na wananchi wameingia katika mtego wa matapeli hawa, hivyo kutekeleza maagizo wanayopewa, ili kupata haki zao ambazo kimsingi hakuna haja ya kutoa rushwa, ili kuzipata .

Mathalani, uhamisho ni haki ya kila mfanyakazi kuhama sehemu moja kwenda nyingine kutumika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale tu anavyokidhi vigezo vya kuhama.

Mtumishi anayo haki ya kulipwa malimbikizo ya madai yake, anayo haki ya kupanda cheo au daraja, anayo haki ya kuteuliwa katika nyadhifa mbalimbali kwa kadri utendaji kazi wake unavyoonekana unafaa, mwananchi ana haki ya kuajiriwa kama amekidhi vigezo vilivyowekwa.

Hayo na mengine ni haki za watumishi na wananchi zisizo na sababu ya wananchi kutoa fedha kwa matapeli wa mitandaoni, ili kuzipata bila kuelewa kuwa kutoa fedha ni kununua haki.

Kukosa subira na kutaka njia za mkato 'shot kat' ili kufanikiwa, kumekuwa kukiwagharamia watumishi wa umma, wastaafu na wananchi na hivyo kushindwa kufanya tafakuri ya kina kabla ya kutekeleza maagizo ya matapeli.

Mara kadhaa ufafanuzi unaotolewa kuwa si maofisa wa serikali wanaofanya vitendo vya utapeli bali ni matapeli wa mitandao wanaojifanya watumishi wa umma kwa kutaka fedha kutoka kwa watumishi, wastaafu na wananchi wenye shida mbalimbali.

> Kibaya zaidi wengine wamekuwa wakilaghai watumishi kwa kutumia jina la Mheshimiwa rais, waziri au maofisa mbalimbali waliopo katika Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa , anatoa tahadhari kutokana na utapeli unaofanywa na matapeli wa mitandaoni kujipatia fedha kutoka kwa watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla, ili waweze kusaidiwa kupata huduma na stahiki mbalimbali.

Sambamba na hilo, Waziri Mchengerwa anakemea matumizi mabaya ya jina la Ofisi ya Rais unaofanywa na matapeli wa mitandao, akisema: "Kibaya zaidi wengine wamekuwa wakilaghai watumishi kwa kutumia jina la Mheshimiwa rais, waziri au maofisa mbalimbali waliopo katika Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma."

Kimsingi, ni wajibu wala si hisani kwa maofisa wa serikali na wale waliopo katika sekta binafsi kuwahudumia wafanyakazi na wananchi wanaohitaji huduma kutoka kwao na kuwapatia haki na stahili zao, bila kutoa rushwa ya aina yeyote.

Kwahiyo, ni wajibu wa watumishi wa umma, wastaafu na wananchi kuongeza umakini na kukataa ushawishi wa matapeli wanapoombwa rushwa, ili kupata haki zao. Serikali kwa upande wao, itimize wajibu wake tena kwa wakati katika kuwapatia watumishi, wastaafu na wananchi stahili na haki zao, ili kutokomeza utapeli unaoweza kufanikiwa kutokana na ucheleweshaji wa haki za watumishi na wananchi.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0620-800462.***

# Mtaala sasa waja mafunzo kuanzia msingi hadi chuo

**INATOKA UK.11**

**DAWA ZILIZOKAMATWA**

Anasema kuanzia Aprili hadi Septemba, mwaka huu DCEA imekamata kilo zaidi ya 900 za heroin na methamphetamine.

Anasema ukamataji huo ni mafanikio makubwa, kwa sababu katika kipindi kifupi hicho mamlaka haijawahi kukamata kiasi kikubwa kama hicho.

Anasema Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) inaeleza kuwa Tanzania imefanikiwa kwa asilimia 90 kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya moja kwa moja.

**NJIA ZA KUINGIZIA**

Kamishna Mfisi anabainisha kuwa njia kuu ya uingiaji wa dawa hizo nchini ni kupitia baharini na zikishafika kunakuwapo na njia nyingi za kuzisafirisha kwenda mataifa mbalimbali kama vile kumeza, kuficha kwenye mikoba, kwenya magogo, usafiri wa ndege na magari.

Anasema dawa za kulevya zinazoingia kwa ndege hapa nchini ni cocaine kwa sababu zinatoka Brazil, ambako haiingiliani na bahari na Tanzania.

Anaongeza:"Kwenye pwani ya Afrika Mashariki dawa zinazoingia kwa urahisi sana, mfano Kenya, Tanzania, Somalia, Msumbiji hadi Afrika Kusini zinatokea Afghanistan. Kisha zinafungwa katika pakiti ndogo ndogo na kupelekwa Hongkong, China na Marekani."

"Kwa mfano kutoka Tanga hadi Mtwara kuna bandari bubu zaidi ya 400, ambazo mtu anaweza kuingiza mzigo pasipo kufahamika, lakini DCEA tunafanya juhudi za kupambana na hali hiyo, tunawakamata kabla hawajazifikia" anasema Dk. Mfisi.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo unyanyasaji unavyotisha japo upo mkakati wa MTAKUWA

LICHA ya taifa kuwa na Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWA), kwa miaka kadhaa, kiwango cha unyanyasaji kwa baadhi ya maeneo kinaacha maswali mengi.

Mathalani, ukatili wa kijinsia (GBV) kama ndoa na mimba za utotoni, ubakaji, vipigo na kutelekezwa kiholela , kwa mfano wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi ni hali inayoelezwa kuwa inakomaa na kuduma.

Wakazi wa baadhi ya Kilwa wanasema sababu za GBV ni pamoja na kukosekana mahitaji muhimu ya kijamii kama chakula, fedha za kujikimu, maji, matibabu, mavazi na mkazi.

Wilayani Kilwa, wanawake na watoto wamekuwa waathirika wa kutafuta huduma za kijamii kama maji usiku na mchana wakiyatafuta kwenye visima, mabondeni , ndani ya madimbwi huku baadhi wakienda hadi kwenye mto Matandu, kwa sababu vijiji vingi havina maji safi na salama.

Wasichana nyakati za usiku hurubuniwa na wanaume kwa ahadi kuwa watawaoa na kuwapa mahitaji muhimu kama maji na kuwahadaa kingono.

Hayo hutokea wakati wa kuchota maji kwenye mabwawa na matokeo yake ni kudanganywa na kuachwa na mimba na kutelekezwa iwapo wamekuwa wakiishi na wanaume hao.

Yote hayo yanatokea licha ya kuwapo MTAKUWA uliolenga kutokomeza GBV ifikapo 2021.

Pili Kuliwa Katibu wa Tumaini Jipya la Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), asasi ya kiraia inayotetea haki za kinamama, kuwahamasisha kuelewa haki zao, kutetea usawa wa kijinsia, kushiriki uongozi, pia kujua mbinu za uwekezaji na kujikomboa kiuchumi.

Taarifa za unyanyasaji zinabainishwa kwa wanahabari waliotembelea Kilwa kwenye miradi ya vijana, wanawake, watoto, elimu na kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi, kuleta usawa wa kijinsia inayofanywa na Shirika la ActionAid.

Pili, anasema lipo ongezeko la GBV na kwamba ukatili huo unaathiri maisha ya jamii kubwa. Familia nyingine hulazimika kuwaoza watoto na TUJIWAKI iliyoundwa kwa kushirikiana na ActionAid Kilwa, imevuruga baadhi ya ndoa za watoto na kuwarejesha masomoni.

Mathalani, umaskini majumbani, anasema unawalazimisha wazazi au walezi kuwatuma watoto kuuza bidhaa usiku kwenye maeneo ya mikusanyiko kazi wanayoifanya wakirejea nyumbani kutoka shule.




Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Mwanaidi Ali Khamis. **PICHA: MTANDAO**

> Taarifa zinaonyesha kuwa linachangiwa na mila na desturi za maeneo hayo kuwa na tabia iliyokithiri ya kuwepo kwa ndoa za msimu hususan wakati wa mavuno ya korosho na ufuta.

Yote haya yanasababisha watoto kubakwa na kudhalilishwa na hasa nyakati za usiku mfano, wavulana wanapokwenda kuuza bidhaa maeneo ya ufukweni hufanyiwa udhalilishaji, kushirikishwa kwenye uhalifu kama kuvuta bangi na dawa za kulevya, anaeleza Pili.

Wazazi na walezi wana mazoea ya kuwaacha watoto nyumbani bila mahitaji muhimu kama chakula, sabuni na fedha matumizi kama kununua dawa wakiumwa, wakienda mashambani kulima ufuta, mpunga na mazao mengine, anasema Anna Komba, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kilwa.

Anafafanua kuwa kukosekana chakula na mahitaji mengine kunachangia watoto wengi kurubuniwa na wanaume wanaowapa mahitaji yanayokosekana na kupata mimba huku wakikatishwa masomo.

Aidha Kamanda Anna, anasema baadhi ya watoto wanalelewa na bibi na babu, ambao wakati mwingine hawawezi kuwafuatilia kwa ukaribu.

Anasema kuna watoto wanalala kwenye vyumba vya mbali au vya uwani hivyo nyakati za usiku wasichana wanakutana na wanyanyasaji wanaowadanganya na matokeo yake ni mimba na hata ndoa za utotoni.

Kamanda Anna, anaungwa mkono na Hamad Abdullah, mwanakijiji cha Maguruwe pia, anayeutaja umaskini ndani ya familia na wazazi kuwaacha watoto kwenda shambani kulima mpunga, ufuta, mbaazi na korosho bila mahitaji muhimu kuwa kunachangia tatizo hilo.

Anasema wazazi au walezi wanakwenda shambani miezi mpaka sita na kuwaacha watoto vijijini bila mahitaji muhimu. Anasema huwaachia mpunga au mtama, lakini hawana sukari, mafuta , sabuni , mboga na fedha za matumizi hivyo wanawalaghai hutumia mwanya huo na kuwarubuni wasichana kingono na wanapopata mimba huwaacha.

Maulid Migomba, mkazi wa Kijiji cha Miguruwe, wilayani humo, anahusisha tabia hizo za kuwatelekeza wenza na kuwaacha watoto kuishi na athari za kisaikolojia na kimwili kuwa ni kukosa maadili, kutokujali utu wa mtu jambo ambalo, limekuwa likijengeka ndani ya jamii.

Anakumbusha kuwa iwapo kijana ambaye ndiye baba wa familia, ilitelekezwa utotoni na kulelewa na bibi au babu yake naye pia ana nafasi ya kutelekeza mkewe na familia yake na ndicho kinachofanyika.

Anasema wazazi walio wengi hawana elimu, hawakusoma kwa hiyo mwamko wa elimu ni mdogo mno miongoni mwao hivyo huwatumikisha watoto katika shughuli za kibiashara mfano kuuza samaki, kalmati na matunda migahawani jioni au maeneo ya uvuvi ufukweni na nyakati za usiku hutokea Watoto kunyanyaswa kingono na wengine hupata mimba.

Baadhi ya maeneo yenye mwingiliano na jamii za wafugaji zinapendelea kuwaoza mabinti katika umri mdogo. Wanavijiji wengine wanasema kukosekana sheria kali za kuwabana wanaotelekeza familia hivyo kuonekana ni jambo la kawaida kwa vile hakuna wanaowajibishwa au kutumikia jela kwa kosa la kutelekeza wake na watoto wao.

Rashid Mchurumbi Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Miguruwe, anasema hali hiyo ni matokeo ya kukosa uadilifu kwa taifa na kwa jamii zao Kwani kutokuwajibika kwa lolote hata kwa watoto unaowazaa mwenyewe.

### KUPATA UFUMBUZI

AKizungumzia ufumbuzi anashauri viongozi wa dini wazungumzie masuala ya maadili kwenye ibada. Aidha, anashauri kuhamasisha kuwapo sharia ndondogo za kulinda watoto na kuwatunza wazazi vijijini badala ya kuacha mambo kubaki kama yalivyo.

Kwa ujumla wananchi hao wanataka utekelezaji wa MTAKUWA ufanyike, usiishie kwenye makabrashi wakati wananawake na watoto wanateseka na GBV

Nipashe imezungumza na Naibu Waziri wa Afya, anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii Mwanaidi Ali Khamis, anasema suala la vitendo vya unyanyasaji wa wanawake na mabinti mfano kubakwa wasichana wadogo,kuozwa usiku na kutelekeza watoto kiholela wilayani Kilwa, serikali imelifuatilia.

Anasema taarifa zinaonyesha kuwa linachangiwa na mila na desturi za maeneo hayo kuwa na tabia iliyokithiri ya kuwepo kwa ndoa za msimu hususan wakati wa mavuno ya korosho na ufuta.

Anasema katika kipindi hicho watu wengi huingia katika ndoa na kuachana pale msimu unapokwisha.

Anawakumbusha wananchi kuwa jukumu la kutokomeza vitendo vya ukatili katika jamii ni kazi ya kila mdau wakiwamo asasi za kiraia, wanahabari, vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi za serikali.

"Tutumie mifumo ya serikali kutokomeza ukatili kwa kutoa taarifa, ili ziweze kushughulikiwa kwa wakati."





# Wanaotoa elimu isiyo sahihi kuhusu matibabu waonywa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, imewaonya watu ambao wamekuwa wakijihusisha na utoaji wa elimu isiyo sahihi na upotoshaji kuhusu magonjwa yasiyoambukiza.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema, hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la watu wanaojihusisha na utoaji wa elimu zisizo sahihi na za upotoshaji kuhusu magonjwa yasiyo ambukiza.

"Elimu hizo zimekuwa zikitolewa kwa njia ya mitandao, hasa zikilenga kutoa ushuru wa lishe, ufanyaji wa mazoezi, kupunguza uzito, matibabu ya magonjwa sugu kama kisukari, saratani na shinikizo la juu la damu," alisema.

Aidha, alisema kwakuwa watoa elimu hao hawana sifa na weledi wanasababisha kuwapo kwa mkanganyiko katika jamii kwa kutoa elimu isiyo sahihi.

"Napenda kutoa rai kwa taasisi, kampuni na wananchi wenye nia njema ya kusaidia serikali kuelimisha jamii ili kuweza kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa ni sahihi," alisisitiza.

Alisema watu wote wanaotoa elimu wanatakiwa kutumia miongozo ya wizara ya afya inayopatikana katika tovuti ya wizara na mitandao ya jamii inayomilikiwa na Wizara ya Afya.

"Pia wanatakiwa kutumia wataalam wenye sifa na weledi katika uelimishaji, kuwasiliana na wizara kupitia kitengo cha mawasiliano serikalini kwa ufafanuzi na uratibu wa taarifa na vipindi, pia kitengo cha elimu ya afya kwa ajili ya kupata vitini vya uelimishaji,"alisema.

Kadhalika, alisema Wizara ya Afya inaendelea kuwakumbusha wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza kwa kufanya mazoezi mara kwa mara kama inavyoshauriwa na wataalam.

"Pia tunawakumbusha wananchi kupunguza matumizi ya chumvi, sukari na mafuta,matumizi ya pombe kuepuka matumizi ya tumbaku na dawa za kulevya,"alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wote kufanya uchunguzi wa awali ili kutambua afya zao na kwa wenye matatizo kuchukua hatua stahiki za kupata matibabu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

# Watoto 35,900 wafanya kazi za mitaani nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani waliopo nchini ni 35,919, hali ambayo ni tishio kiusalama kutokana na baadhi yao kujiingiza kwenye makundi ya kihalifu.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa kikao cha kujadili tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani kilichofanyika jijini hapa.

Alisema watoto hao ni kundi kubwa wanakaa mitaani katika Majiji na Miji mbalimbali nchini na wamekuwa wakijilea wenyewe na wakati mwingine wakilelewa na watu ambao mienendo na tabia zao haikubaliki kwa jamii na kulazimika kujiingiza kwenye makundi ya kihalifu ikiwamo uhalifu wa kimataifa.

"Ni tatizo la ustawi na maendeleo ya jamii kokote linapokuwapo nchini kwetu kwenye mikoa yetu hasa kwenye Majiji na Miji yetu tunao watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, kwa mujibu wa taarifa ya wenzetu wa TAMISEMI, watoto hawa sasa wapo 35,919 wanapungua na kuongezeka," alisema.

Alisema watoto hao wakiendelea kukaa mitaani litatengenezwa tatizo kubwa katika ustawi na maendeleo ya jamii kwa kuwa watakuwa hawajapata maadili na malezi kwa kujilea wenyewe.

"Ukienda Dar es Salaam watoto wanasema wanakaa na watu wanaowaita mabrother ni wahalifu wale, ndio wanaowalea, wanawaongoza nini cha kufanya na kipi ambacho si cha kufanya, watoto wanaolelewa na hawa mabrother hawa nao wanakuwa wahalifu, ni tatizo la kijamii na kiusalama," alisema.

Alisema suala hilo ni tatizo na halikubaliki na lazima lifanyiwe kazi.

Katibu huyo alisema kikao hicho kitajadili kwa kina suala hilo na kubaini chanzo cha uwapo wa watoto hao mitaani.

Kwa upande wake, Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Shilungu Ndaki, alisema kikao hicho kinalenga kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo ambalo ni kubwa.

"Tatizo la watoto wanaoishi mitaani ni kubwa, watoto wameendelea kuongezeka mitaani kutokana na wazazi na walezi kutowajibika... ukatili unaongezeka, migogoro ya ndoa inasababisha kuongezeka kwa watoto hao," alisema.

Alisema hadi kufikia Mach, mwaka huu watoto 1,506 wameunganishwa na familia huku akisema zaidi ya asilimia 90 ya watoto hao wazazi au walezi wao wanafahamika wanapoishi.

Awali, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika lisilo la kiserikali la PACT Tanzania, Mariana Balampama, alisema moja ya afua muhimu ambayo wanatekeleza na shirika hilo ni kutokomeza tatizo hilo kwa kuwatambua, kuwarejesha shuleni, kuwapatia mafunzo ya ufundi stadi na kuunganisha na familia.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zaidi ya watoto 8,300 wamefikiwa kwa kushirikiana na mashirika mengine huku akisema suluhisho la kudumu la tatizo hilo linahitaji ushirikiano mkubwa wa sekta mbalimbali.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, akionyeshwa ramani ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Kanda kilichopo Nala jijini Dodoma wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua ujenzi unaoendelea.**PICHA: RENATHA MSUNGU.**

# Kifua kikuu chaendelea kuwa tishio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini wamefikia 1,600 hivi sasa, huku watu 74 wanakufa kila siku kutokana na ugonjwa huo.

Akizungumza juzi kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Saitole Laizer, kwenye uzinduzi wa muungano wa wadau wa kupambana na kifua kikuu nchini, alisema vifo hivyo ni sawa basi moja la abiria.

"Kwa idadi hiyo, ni sawa na idadi ya abiria wanaosafiri katika basi lenye uwezo wa kubeba watu 65 hadi 70 ambao wangeweza kukaa katika siti na wengine kusimama," alisisitiza Dk. Laizer.

Alisema sababu kubwa ya ugonjwa huo ni kushuka kwa kinga kupita kiasi pia watu wenye matatizo ya ugonjwa sukari,saratani na utapiamlo mkali wapo katika kundi hatarishi.

"Hivi sasa wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini wamefikia 1,600 na katika kipindi cha mwaka jana pekee waligundulika wagonjwa wa kifua kikuu sugu 443," alisema Dk. Laizer.

Dk. Laizer alisema moja ya vikwazo vinavyochangia kuwapo kwa idadi hiyo ya wagonjwa ni pamoja na kutoyafikia makundi yaliyomo katika hatari kama vile watumiaji wa dawa za kulevya.

"Tunashukuru hivi sasa serikali imetoa fedha nyingi ambazo zimefanikisha kununua magari mapya matano kila moja kwa Sh.milioni 80, yatakayofanya kazi hadi vijijini kwa ajili ya kufanya vipimo kwa watu wanaoshindwa kufika hospitalini," alisema Dk. Laizer.

Naye, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Godwin Mollel, alisema Wizara imepokea Sh. bilioni 97 kwa ajili ya kupambana na maambukizi ya kifua kikuu ikiwamo kuimarisha huduma za afya vijijini.

Alisema, wanatarajia kuwafikia watu wengi kwa kutumia magari hayo kama Kliniki tembezi, hali ambayo inakwenda kumaliza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo kwa kupeleka elimu moja kwa moja kwa jamii ilikufikia azma ya serikali ya kutokomeza TB ifikapo 2030.

Akizindua Umoja huo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema TB ni miongoni mwa magonjwa yanayoua kwa wingi nchini hivyo mapambano yake hayatakiwi kufanyiwa mzaha.



# Wakulima mpunga kuchangia gharama umwagiliaji Mbarali

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika skimu ya Mwendamtitu wilayani Mbarali, wametakiwa kuchangia gharama za uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya skimu hiyo ili iwasaidie kuondokana na tatizo la uhaba wa maji unaosababisha mazao yao kukauka.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Kilimo anayeshughulikia mazao wilayani Mbarali, Jamson Mwailana kwenye Madhimisho ya Siku ya Mkulima wa Mpunga wilayani humo yaliyofanyika katika Kijiji cha Mwendamtitu wilayani humo.

Alisema katika skimu hiyo kila mwaka unatokea ukame ambao unaathiri mazao yao kutokana nna mchanga kuziba mfereji na kusababisha maji yasifike kwenye mashamba ya wakulima na wakati mwingine usafishaji wa mfereji kuchelewa kutokana na wakulima hao kutochangia gharama.

"Kilimo kinahitaji teknolojia na miundombinu rafiki msitegemee tu mvua kwenye uzalishaji wa mpunga tafuteni vyanzo vingine vya maji ili msimu ujao mpate mavuno mengi," alisema Mwailana.

Alisema wakulima hao ndiyo wanufaika wa skimu hiyo na wanatakiwa kushiriki kuihudumia ili iwasaidie kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi wao pamoja na kuwa na uhakika wa chakula.

Mratibu wa skimu hiyo, Bruno Mgumba, alisema gharama wanazopaswa kuchagia wakulima hao ni Sh. 50,000 kwa kila ekari moja na zimepangwa na serikali.

Alisema serikali ilipanga gharama hizo kwa kuzingatia bei ya chini ya mpunga ambayo sawa na bei ya gunia moja.

Alisema gharama ya uendeshaji wa skimu za umwagiliaji ni kubwa katika baadhi ya maeneo, lakini kwa Wilaya ya Mbarali skimu nyingi gharama zake ni za kawaida kutokana na jiografia yake kuwa ya tambarare maeneo mengi.

"Asilimia 70 ya gharama hizo hutumika katika kukarabati miundombinu ya skimu hii na asilimia 30 hutumika kwenye uendeshaji, tatizo ambalo huwa linatokea ni baadhi ya wakulima kutochangia kwa wakati na wengine kutochangia kabisa," alisema Mgumba.

Baadhi ya wakulima wanaotumia skimu hiyo walisema wakulima wenyeji huwa wanachangia, lakini tatizo huanzia kwa wakulima wageni ambao huwa wanakodi mashamba ama kuyanunua kutoka kwa wenyeji.

Mmoja wa wakulima hao, George Morice, alisema wengi wao huwa siyo waelewa na kushindwa kukubali kuchangia gharama za uendeshaji wa skimu na kuwaomba viongozi wa serikali watoe elimu zaidi kwa wakulima hasa msimu wa kulima ambao kila mkulima anapatikana mashambani.

Alisema kutokana na mfereji wa skimu hiyo ulivyo pamoja na miundombinu yake bado gharama ya Sh. 50,000 ni ndogo na hazitoshi kuendesha skimu.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Dk. Vicent Anney, akizungumza na Umoja wa Wakulima wa Parachichi Rungwe (UWAMARU) pamoja na Shirika la United State African Development Foundation (USADF) ambapo wametia sahihi makubaliano ya kuzalisha na kuongeza tija uzalishaji wa zao hilo juzi. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Wanawake wajikomboa kwa kujenga nyumba zao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 60 ya wanawake mkoani Mbeya, wamefanikiwa kujenga nyumba zao wenyewe kutokana na juhudi walinazo katika kufanya kazi kwa bidii.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mbeya, Stela Kategile akizungumza na Nipashe jana, alisema asilimia kubwa ya wanawake mkoani humo wanaendesha maisha yao bila kutegemea msaada wa mwanamume na wamefanikiwa kumiliki nyumba zao.

Alisema nyumba zilizojengwa na wanawake ambao kwa kiasi kikubwa ni wajasiriamali zinavutia kwa sababu zimezingatia ubora na kiwango kinachotakiwa kwa kuzingatia ramani ya mipango miji inayotolewa na serikali.

Kategile aliwapongeza wanawake hao kwa kukubali kupunguza mambo yasiyofaa na kuamua kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba akieleza ni urithi usioharibika na kwa vizazi vijavyo.

"Wanawake wa Mbeya ni miongoni mwa wanaojituma sana katika kutafuta riziki, wanajishughulisha na mambo mbalimbali ili kujiongezea kipato ukilinganisha na wanaume ambao asilimia kubwa wanapenda kulelewa, ukionyeshwa nyumba inayomilikiwa na mwanamke utashangaa kwa sababu ya uzuri wake, hakika tuige mfano wao," alisema Kategile.

Aliongeza kuwa kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na ukuaji wa miji, wananchi wanapaswa kujenga nyumba za kisasa ambazo zinavutia miji kuliko ilivyo sasa katikati ya Jiji la Mbeya zimejengwa nyumba za ovyo.

Aliwashauri maofisa mipango miji kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaonunua ardhi kuhakikisha wanafuata ramani zinazotolewa kujenga nyumba za kisasa badala ya kujiamulia kutumia michoro yao.

Baadhi ya wanawake walisema kuwa siri ya kumiliki nyumba nzuri na za kisasa ni kufanya kazi kwa bidii na kubana matumizi ya fedha inayopatikana.

Miongoni mwao akiwamo Salome Anangisye, mkazi wa Isyesye jijini hapa, alisema baadhi yao wanapenda vitu vya anasa na wanasahau kuwa binadamu anatakiwa kula, kuvaa na kuishi mahali pazuri pa kuvutia.

Alisema miongoni mwa faida za kumiliki nyumba ni kuondokana na msongo wa mawazo kutokana na madeni ya kodi kwenye nyumba za kupanga na kupata amani ya moyo na hewa safi.

# Viongozi CCM kuanzisha miradi ya kuingiza kipato

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMATI ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imewasisitiza viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi zote kuanzisha miradi itayowawezesha kuingiza kipato ili wafanye kazi kwa uadilifu katika kutatua kero za wananchi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Jacob Mwakasole, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe jana kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama hicho ili kuwakwamua kiuchumi.

Alisema jukumu la viongozi hao ni kusikiliza kero za wananchi na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika ili zitatuliwe, lakini wasipokuwa vizuri kiuchumi na wao wanaweza wakawa wanaingia kwenye mitego isiyokuwa na sababu.

Mwakasole aliwataka viongozi hao pia kusimamia kwa ukaribu miradi ya chama ili kuhakikisha haihujumiwi na watu wenye nia ovu na kukisababishia chama hasara.

"Sisi viongozi ndiyo wa kuwasaidia wananchi wetu, lakini kama huko vizuri kiuchumi niwahakikishie kabisa, huwezi hata siku moja ukatekeleza majukumu yako vizuri, kwahiyo nawashauri sana muanzishe miradi," alisema Mwakasole.

Akitoa taarifa ya miradi mbalimbali ya serikali inayotekelezwa wilayani humo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema miradi hiyo inaendelea vizuri ikiwamo ujenzi wa barabara ya Chunya-Makongolosi kwa kiwango cha lami.

Alisema barabara hiyo inakaribia kumalizika na ikikamilika itakuwa imefungua fursa kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo kufanya shughuli zao ikiwamo biashara ya mazao.



## Serikali yakamilisha upokeaji walimu mpango wa ugatuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema tayari imekamilisha mchakato wa kuwapokea walimu wote ambao awali walikuwa katika mpango wa ugatuzi katika serikali za mitaa ikiwamo masuala ya maslahi yao.

Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohamed Said, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Pemba, Shamata Khamis Shaame, aliyetaka kujua utaratibu wa kuwapokea wanafunzi baada ya kufutwa kwa mpango wa ugatuzi.

Waziri Said alisema serikali imefuta mpango wa ugatuzi baada ya kubainika ufanisi wa utekelezaji usioridhisha ikiwamo kuwapo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi hadi suala la maslahi ya posho.

Alisema tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekamilisha mchakato wa kuwapokea wafanyakazi wote kutoka Wizara ya Elimu msingi na maandalizi ikiwamo walimu kutoka serikali za mitaa.

Alizitaja hatua hizo ni kukamilisha usajili wa masuala ya maslahi pamoja na kuwaingiza katika taratibu za mfuko wa hifadhi ya jamii na kumbukumbu zake zote.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021-2022 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejikita zaidi kuimarisha mitaala ya elimu na tayari wananchi na wadau wa sekta ya elimu wamepata nafasi ya kutoa maoni yao.

Alisema miongoni mwa malalamiko yaliyotolewa na wazazi ni kasoro za mitaala ya elimu ikiwamo kuwapo kwa kwa kasoro kubwa ya masomo mengi kwa wanafunzi wa msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la sita ambayo yana jumla ya masomo nane.

"Kazi kubwa inayofanywa na wizara yangu kwa sasa ni kufanya marekebisho ya mitaala ya elimu ya msingi na maandalizi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kwa muda mrefu kiasi ya kushuka kwa ufaulu katika hatua za awali," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefuta mpango wa ugatuzi katika sekta tatu ikiwamo elimu ya msingi, kilimo na afya kutoka serikali za mitaa na halmashauri na sasa kusimamiwa na wizara mama kwa lengo la kuleta ufanisi wa utoaji huduma bora.

# Uchumi wa bluu wapigiwa debe nchi za jumuiya IORA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Joseph Sokoine, amewataka washiriki wa kikao kazi cha wadau wa jumuiya ya nchi zilizopo kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA), kujadili kwa kina na kuweka mapendekezo yatakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa bluu, sheria kanuni na taratibu za kuvuna na kuhifadhi rasilimali zilizopo kwenye bahari hasa katika ukanda wa bahari kuu.

Aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akifungua mkutano wa wadau wa jumuiya ya nchi IORA ambao wadau hao wana kikao cha siku tatu ikiwamo kutembelea vivutio vya utalii.

Alisema ni lazima kujadili kwa kina sera na muongozo wa kufanikisha utekelezaji wa uchumi wa bluu pamoja na umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya bahari kwa maendeleo endelevu na usalama wa eneo la bahari.

Alisema kwa bahati nzuri Tanzania haina deni kwenye jumuiya ya IORA na kwamba ni mafanikio makubwa katika kuimarisha ushiriki wa Tanzania kwenye jumiya hiyo kwa kuzingatia vigezo vya kuandaa na kuomba ufadhili wa miradi kwa maslahi ya kanda na nchi zilizomo katika jumuiya.

Alizitaka wizara na sekta mbalimbali kuandaa mapendekezo ya miradi yenye sifa na vigezo ya kupatiwa ufadhili kwenye mfumo maalum wa IORA ili kusaidia kuwezesha na kuhudumia wananchi.

"Naendelea kusisitiza kuwa miradi hiyo lazima ilenge uwezeshaji wa jamii ya maeneo inayozunguka ukanda wa bahari, kulenga maeneo ya uhifadhi wa bahari na uvunaji endelevu wa rasilimali za bahari, uwezeshaji wananchi kiuchumi na maeneo mengine yenye maslahi ya wananchi," alisema.

Alisema majukumu na malengo ya jumuiya hiyo ni kulinda na kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari, kuimarisha uwekezaji na biashara, kuendeleza na kukuza sekta ya utalii na utamaduni, kuimarisha elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu, kukubaliana na majanga katika Bahari ya Hindi, kuendeleza na kuimarisha ushirikiano katika uchumi wa bluu, kuimarisha sekta ya uvuvi hasa katika uvuvi wa bahari kuu na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Alisema katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya jumuiya hiyo imeunda vikundi kazi vyenye jukumu la kuchakata, kuandaa, kutathmini na kufuatilia malengo ya utekelezaji wa IORA.

"Jumuiya hiyo ina vikundi kazi vinane vinavyogusa wizara na sekta mbalimbali ambavyo ni kikundi kazi cha ulinzi na usalama wa bahari, biashara na uwekezaji, utalii na utamaduni, elimu sayansi, teknolojia na ubunifu cha kukabiliana na maafa, uchumi wa bluu, uvuvi na uwezeshaji wananchi kiuchumi," alisema Balozi Sokoine.

Pia, alisema kuna haja ya kuunda upya na kuimarisha vikundi kazi vilivyopo katika jumuiya hiyo ili viendane na utendaji kazi.

Naye Mkurugenzi Idara ya Ushirikiano wa Kikanda, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Agnes Kayola, alisema jumuiya ya nchi zilizopo kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi inaundwa na nchi 23 ambazo zi Australia, Afrika Kusini, Bangladesh, Comoro, India, Indonesia, Iran, Kenye, Madagascar, Malaysia, Maldieves, Msumbiji, Mauritius, Oman, Ufaransa, Seychelles na Singapore, Somalia, Srilanka, Thailand, Umoja wa Falme za Kiarabu, Yemen na Tanzania.

Alisema tangu kuanzishwa kwa jumuiya hiyo mwaka 1997, Tanzania haijawahi kugombea nafasi yoyote ya uongozi na kwamba wakati umefika kuona umuhimu wa kushiriki kikamilifu kwenye jumuiya hiyo ikiwa ni pamoja na kushika nafasi za uongozi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ofisi za Zanzibar, Balozi Masoud Abdallah, alisema wajumbe wa mkutano huo kutoka pande mbili za Muungnao wa Tanzania watapata fursa ya kutembelea vivutio vya kitalii ikiwamo samaki aina ya pomboo katika Bahari ya Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, akijibu swali aliloulizwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Muswada kuanzishwa Ofisi ya Msajili Hazina waiva

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamali Kassim Ali, amewasilisha mswada wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na usimamizi wa mali za umma ambayo itahakikisha mashirika na taasisi hizo zinafanya kazi zake na kuleta tija kwa taifa na kukuza uchumi pamoja na kutoa gawio la mgawo Serikali Kuu.

Alisema hayo wakati akiwasilisha mswada huo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, ambao unafuta sheria ya mitaji ya umma ya mwaka 2004 namba nne na kuanzishwa kwa sheria mpya ambayo imelenga kuleta ufanisi wa mashirika ya umma kuleta tija.

Akifafanua alisema serikali imekuja na sheria mpya ambayo itahakikisha mashirika ya umma yanakuwa tegemeo katika kukuza uchumi na kuongeza pato la taifa.

Alisema sheria hiyo mpya inayopendekezwa lengo lake kuleta ufanisi wa kuyasimamia mashirika ya umma ikiwamo kuleta gawio la serikali na faida.

"Huu ni mswada mzuri ambao umekuja kwa wakati muafaka wa kuhakikisha mashirika na taasisi za umma zinatekeleza majukumu yake ikiwamo kutoa gawio serikalini ikiwa ni sehemu ya malengo yake," alisema.

Waziri Jamal alisema sheria iliyopo sasa ni dhaifu ambayo haitoi nafasi nzuri ya kuyasimamia mashirika ya umma kikamilifu ikiwamo kutoa gawio serikalini na kuongeza ubunifu pamoja na ajira.

Alisema sheria inayofanyiwa marekebisho ya mitaji ya umma ya mwaka 2002 ilikuwa na jumla ya vifungu 35 pekee ambavyo havitoshi ikiwa na upungufu mkubwa na kasoro na kwamba mswada unaowasilishwa mbele ya baraza una jumla ya vifungu 81.

Pia, katika sheria mpya inayopendekezwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, sasa itayawezesha mashirika ya umma ya serikali kuongeza ufanisi katika uzalishaji na ubunifu na kuwa tegemeo la mapato na uchumi.

Alisema sheria mpya sasa itayafanya mashirika ya umma kuwa yenye ufanisi wa hali ya juu kwa watendaji wake na watakaoshindwa watalazimika kukaa pembeni.

"Huu ni mswada muhimu ambao sasa unakwenda moja kwa moja kusimamia mashirika ya umma kuleta ufanisi wa uzalishaji mali na taasisi hizo kuwa na tija," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**BENJAMEN KIMAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0475/0036 kilichotolewa na **KIDIA SEKONDARI** mwaka **1999**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: MOS/RB/730/2010**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORIAN NESTORY NJUNWA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA **USAJILI T 251 BTF. CHASSIS NAMBA MR 515604323. ENGINE NAMBA M13A1115442.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/441360/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SADAT BARAKAT SALEH** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 171 BSP.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/440261/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMMED AMOUR DUGHEISH** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 837 CQA.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/440788/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.285/2021**

Ombi la **SAMIA MTORO MKUDE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ISMAIL ATHUMAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 13/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.279/2021**

Ombi la **FANUEL MUKAMA TANDA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **PHILIMON BARAOYE MKAMA TANDA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 12/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUMI FELEMON KWEKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE COMMUTER** yenye namba za usajili **T 718 DCZ. Chassis No. RZH1331002363, Engine No. 2RZEAA2363.**Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/441855/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CONSOLATHA DEUSDEDIT KADIKILO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T 826 DLG. Chassis No. ACU300020561, Engine No. 2AZ1481408.**Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/440182/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**PASCHAL JOSEPH DUWAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya Trekta aina ya **TRECTOR FORD** yenye namba za usajili **T679DDT,** Chasisi namba **EA314C5G08BA60702,** Engine namba **E497537.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **MAN/BAB/RB/438126/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FALY DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 693 BUP** aina ya **BOXER.** Yeyote akaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya Jeshi la Polisi **MAJ/RB/1588/2021.**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA**
**SHAURI LA MIRATHI NO 17/2021**
**MWOMBAJI............JUDITH KANZANILA**
**MAREHEMU......GERAL OTIENO NJURA**

**KWA: YEYOTE ANAEHUSIKA**

**KUITWA SHAURINI**
Mwombaji tajwa hapo juu amefungua shuri la mirathi ya marehemu **GERAL OTIENO NJURA** katika mahakama hii hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.
Tunaomba yeyote mwenye pingamizi katika mirathi hii anatakiwa kuhudhuria mahakamani tarehe 01/10/2021 saa 2:00 asubuhi ninyi/ wewe binafsi au wakili wenu kisheria.
**Zingatia** kwamba kutohudhuria kwenu kwa tarehe tajwa, kesi hii itaendelea bila nyinyi kuwepo mahakamani.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 06/09/2021.

HAKIMU MKAZI
WILAYA YA NYAMAGANA
MWANZA

**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA.**
**MWANZA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO ARUSHA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI**
**NA. 492/01 YA 2019**
**CATHERINE HONORATI...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. CRDB BANK**
**2. METHOD KAUNGA MORIS**
**3. HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE.............WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**1. METHOD KAUNGA MORIS**
**2. HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE**

**POPOTE MLIPO**
Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii Arusha tarehe 29 Septemba, 2021 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria basi maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.
Imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 26/08/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORIAN NESTORY NJUNWA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA **USAJILI T 251 BTF. CHASSIS NAMBA MR 515604323. ENGINE NAMBA M13A1115442.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/441360/2021.**




NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mwanamke wa kwanza kuwania urais Somalia

**Mogadishu. SOMALIA**

MWANAMKE wa kwanza ambaye amevunja vikwazo na kuwa waziri wa mambo ya nje pamoja na naibu waziri mkuu, sasa analenga kuwania urais, kwenye uchaguzi mkuu ambao umecheleweshwa kwa muda mrefu.

Fawzia Yusufu H. Adam anafahamu vyema vikwazo vinavyomkabili kupata uungaji mkono kwenye taifa ambalo mara nyingi linawabagua wanawake.

Ingawa wanawake wengi wamesoma kwenye mataifa ya kigeni, na sasa wanarejea Somalia, ili kuchangia kwenye ujenzi wa taifa baada ya mapigano ya miongo mitatu, kukubalika kwa mwanamke kama rais bado ni tatizo.

Wakati akifanya mahojiano na shirika la habari la AP, Fawzia alisema kwamba hata kuongoza wafanyakazi kwenye wizara ya mambo ya nje ambapo wafanyakazi wengi ni wanaume ni kikwazo, akiongeza kuwa baadhi wanakataa kutoa ushirikiano kwake kutokana na kuwa yeye ni mwanamke.

Alisema kwamba baadhi ya marafiki zake hawaamini anaweza kuongoza taifa hilo, kutokana na jinsia yake.

Abdiwahid Mohamed Adam ambaye ni daktari kwenye hospitali mojawapo mjini Mogadishu, alisema kwamba Fauzia ni kiongozi mzuri kwa bahati mbaya ni mwanamke ambaye hawezi kukubalika kirahisi nchini mwake.

**VOA**



Mwandamanaji akikabiliana na polisi wa kutuliza ghasia wakati wa maandamano dhidi ya vizuizi vilivyowekwa nchini Ufaransa pamoja na kukabiliana na janga la Covid-19, jijini Paris, jana. **PICHA: REUTERS**

## Mke TB Joshua amrithi mumewe kuongoza kanisa

**Lagos, NIGERIA**

KANISA la Sinagogi ama SCOAN, limemteua mke wa TB Joshua, Nabii Evelyn Joshua kuwa kiongozi mpya wa kanisa hilo.

Kanisa limesema katika taarifa yake kwenye ukurasa wa Facebook kuwa programu nzima ya kanisa itakuwa chini ya uongozi wa Mungu kwa maelekezo ya Evely Joshua.

Kwa mujibu wa chapisho hilo, wakati ulikuwa sahihi na wafuasi wa kanisa waliombwa wasali kwa ajili ya Utukufu wa Mungu.

Awali kulikuwa na tetesi kuhusu nani atakayeongoza kanisa baada ya mwanzilishi wa kanisa TB Joshua, kuaga dunia Mei, mwaka huu.

Mabishano hayo yalisababisha kufukuzwa hivi karibuni kwa baadhi ya wafuasi wa TB Joshua kanisani.

Huduma ya TB Joshua, ilitangaza kuwa mwanzilishi wa kanisa hilo na nabii mkuu wa Nigeria, Temitope Balogun Joshua amejiuzulu kwenye ukurasa wake wa Facebook, Jumamosi Juni 5, mwaka huu.

**BBC**

## Taliban yaweka amri wanafunzi wa kike kutengwa na wavulana

**Kabul, AFGHANISTAN**

CHUO Kikuu cha Afghanistan, kitatenganishwa kwa jinsia na aina mpya ya mavazi yatatambulishwa, imesema Taliban.

Waziri wa Elimu ya Juu, Abdul Baqi Haqqani, ameeleza kuwa wanawake wataruhusiwa kusoma ila hawatasoma pamoja na wanaume.

Pia alitangaza masomo ambayo yatakuwa yanafundishwa.

Wanawake na wasichana walipigwa marufuku kusoma shule na vyuo chini ya sheria ya Taliban kati ya mwaka 1996 na 2001.

Taliban ilisema haitazuia wanawake kupata elimu au kuwa na ajira. Tangu wamechukua taifa hilo Agosti 15, mwaka huu, wamewataka wanawake wote isipokuwa wale wanaofanya kazi katika sekta ya afya kutofanya kazi mpaka hali ya kiusalama itakapoimarika.

Tangazo la Jumapili kuhusu sera ya elimu ya juu, limejiri siku moja baada ya Wataliban kupandisha bendera yao katika Ikulu ya rais, ikionyesha ishara ya mwanzo wa utawala wao.

Wanafunzi wasichana walikuwa hawapewi kipingamizi cha mavazi na vyuo vikuu vilikuwa na wanafunzi mchanganyiko wanaume kwa wanawake.

Lakini bwana Haqqani hakuonesha kusikitishwa na maamuzi hayo. "Hatuna tatizo katika kusitisha mfumo wa elimu ya mchanganyiko," alisema. "Watu wetu ni waislamu hivyo watakubali."

Wasichana na wavulana pia watatengwa katika shule za msingi na sekondari, kitu ambacho kilikuwa kimezoeleka Afghanistan kote.

Wanawake watatakiwa kuvaa hijabs, hata hivyo bwana Haqqani hakufafanua kama itakuwa lazima kuwa hijabu za kufunika uso au la.

Waziri mpya aliyewekwa alisema masomo ambayo yatafundishwa chuo kikuu yatapitiwa upya.

"Aliwaambia waandishi kuwa Taliban inataka kutengeneza mtaala unaofaa na wa Kiislamu kulingana na Waislamu wetu," maadili ya kitaifa na ya kihistoria na kwa upande mwingine, kuweza kushindana na nchi zingine.

**BBC**

## Hati ya Covid-19 kutumika safari zote za Afrika Kusini

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa, ametangaza nia yake ya kuanza kutumika kwa Hati ya kusafiri ya Covid-19, huku wengi wakipuuzia kuchanjwa dhidi ya ugonjwa huo, katika nchi iliyoathiriwa zaidi na virusi vya corona barani Afrika.

Katika hotuba kwa taifa kwa njia ya televisheni mwishoni mwa wiki, rais Cyril Ramaphosa alihakikisha kuwa chanjo kwa watu wazima, ilikuwa sharti la lazima kufungua tena uchumi na kuepusha mlipuko wa nne wa maambukizi.

"Katika wiki mbili, tutatoa habari zaidi juu ya mfumo wa hati ya kusafiri ya chanjo ambayo inaweza kutumika kama uthibitisho wa chanjo kwa madhumuni mbalimbali na katika hafla mbalimbali," Cyril Ramaphosa alisema bila kutoa maelezo zaidi.

Aliongeza kuwa "kushuka kwa visa vya maambukizi kwa wiki chache zilizopita ingewezesha, hata hivyo, kulegeza hatua za kudhibiti virusi vya corona kuanzia Jumatatu."

Muda wa sheria ya kutotoka nje usiku utaongezwa kwa saa moja hadi saa tano usiku na idadi ya watu kukusanyika itaongezwa.

Vizuizi dhidi ya uuzaji wa pombe pia vitalegezwa, ingawa barakoa zitabaki kuwa lazima katika sehemu zilizo wazi kwa umma.

**RFI**

## Ujumbe wa ECOWAS wataka usalama wa Condé

**Conakry, GUINEA**

UJUMBE kutoka Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), umekuwa na mkutano wa kwanza na wanamgambo wa junta katika mji mkuu, Conakry.

Wanadiplomasia, wakiwamo mawaziri wa kigeni kutoka Ghana, Burkina Faso na Togo, walifika nchini humo kufuatia mapinduzi dhidi ya Rais Alpha Condé.

Katika kujibu, ECOWAS, ililaani mapinduzi na kuiondoa Guinea katika jumuiya hiyo.

Ujumbe huo, ulitaka kuhakikishiwa kwamba rais Condé yuko katika afya njema, kushinikiza kuachiliwa kwake kutoka mahabusu na kuomba ratiba ya kurejea kwa utekelezwaji wa mfumo wa katiba.

**BBC**

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499

MECHI KALI
HOME
AWAY
BARCELONA
3.40 | 4.00 | 1.94
BAYERN MUNCHEN

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888,
KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# INZAGHI AJUTIA INTER KUPATA SARE NYINGINE



**MILAN,** Italia

SIMEONE Inzaghi ana "jutia" baada ya Inter Milan kupata sare ya pili mfululizo wakati Jumapili ikitoka 2-2 na Sampdoria katika mchezo wake wa 200 katika Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa kocha.

Mabao ya Federico Dimarco na Lautaro Martinez yaliifanya Inter kuonekana kama wataibuka na ushindi kwenye mchezo huo uliopigwa uwanja wa Luigi Ferraris.

Hata hivyo, bao la kujifunga la Edin Dzeko na lile la Tommaso Augello yakaiwezesha Sampdoria kuondoka na pointi kwenye mchezo huo na kuwafanya Inter kuambulia sare ya pili mfululizo kwenye Serie A.

"Kuna majuto mengi, kwa sababu ni mchezo ambao tulitakiwa kushinda," alisema Izaghi akiiambia Sky Sport Italia.

"Timu yetu ilichukua uongozi mara mbili, halafu makosa ya Ivan Perisic na Hakan Calhanoglu yakatukosesha ushindi.

"Tuliruhusu mabao mawili, moja lilikuwa la kujifunga kwa Edin Dzeko, lingine tukifungwa na Tommaso Augello, lakini tulitakiwa kushinda.

"Tulicheza dhidi ya timu nzuri na ilikuwa imejipanga vizuri sana, lakini majuto mengine ni kwamba, Sensi aliumia na tulimaliza mchezo tukiwa na wachezaji 10 uwanjani."

# KLOPP: KUUMIA KWA ELLIOTT NI PIGO




**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema nyota wa Liverpool, Harvey Elliott alikuwa kwenye "maumivu makubwa" baada ya kuumia vibaya 'enka' (kifundo cha mguu) kwenye mchezo wa ushindi wa 3-0 dhidi ya Leeds United, Jumapili.

Elliott mwenye umri wa miaka 18, alibebwa kwenye machela uwanjani na kukimbizwa hospitali baada ya kuchezewa vibaya na mlinzi wa Leeds, Pascal Struijk, ambaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Klopp alisema Elliott kifundo chake cha mguu kiligeuka baada ya kuumia kwenye mchezo huo.

"Tutacheza bila yeye, lakini tutamsubiria yeye kwa sababu ni mchezaji mkubwa," aliongeza kocha huyo wa Liverpool.

Taarifa zaidi kutoka Liverpool zinasema nyota huyo wa zamani wa Fulham ameshatoka hospitali, lakini atahitaji kufanyiwa operesheni kwa siku zijazo.

"Harvey, familia yake na Liverpool FC ingependa kutoa shukrani kwa timu ya madaktari wote pamoja na wale wa Leeds kwa huduma ya haraka," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Tunamtakia apone haraka na arudi uwanjani kwa wakati."

Kwenye mchezo huo, fowadi Mohamed Salah alifunga bao lake la 100, kwenye Ligi Kuu England.



HABARI MICHEZO

,059,740

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 18.9.21 | 17:00 | Derby vs Stoke City | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 2. 18.9.21 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 3. 18.9.21 | 17:00 | Cardiff vs Bournemouth | 2.86 | 3.31 | 2.36 |
| 4. 18.9.21 | 17:00 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 5. 18.9.21 | 18:00 | Lens vs Lille | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 6. 18.9.21 | 19:30 | Aston Villa vs Everton | 2.46 | 3.27 | 2.92 |
| 7. 18.9.21 | 19:30 | Elche vs Levante | 2.67 | 3.13 | 2.77 |
| 8. 18.9.21 | 22:00 | Alaves vs Osasuna | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 9. 19.9.21 | 13:30 | Empoli vs Sampdoria | 2.52 | 3.63 | 2.62 |
| 10.19.9.21 | 14:00 | Nice vs Monaco | 2.73 | 3.38 | 2.48 |
| 11. 19.9.21 | 16:00 | Brighton vs Leicester | 2.83 | 3.19 | 2.58 |
| 12. 19.9.21 | 17:15 | Real Sociedad vs Sevilla | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 13. 19.9.21 | 21:45 | Juventus vs AC Milan | 2.36 | 3.32 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 14 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2467 | Campbelltown City vs Adelaide Olympic | 1.63 | 4.05 | 4.25 |
| 14:00 | 3427 | Ulsan Hyundai vs Kawasaki Frontale | 2.42 | 3.25 | 2.67 |
| 14:15 | 1347 | Kokand 1912 vs Mash AL Mubarek | 1.62 | 3.49 | 5.24 |
| 16:30 | 5431 | Bandirmaspor vs Eyupspor | 2.16 | 3.40 | 3.30 |
| 17:00 | 3434 | ACS Sirineasa vs Hermanstadt | 3.62 | 3.04 | 2.04 |
| 17:30 | 2425 | Maccabi Haifa vs Feyenoord | 3.10 | 3.44 | 2.07 |
| 17:30 | 5564 | Maccabi Tel Aviv vs Alashkert Martuni | 1.28 | 4.73 | 9.64 |
| 18:30 | 1272 | FC KTP vs Seinajoen JK | 6.19 | 4.16 | 1.44 |
| 18:30 | 4086 | Ilves Tampere vs Hifk | 2.85 | 3.14 | 2.35 |
| 19:00 | 4894 | Al Nasr Riyadh vs Teraktor Sazi | 1.21 | 6.01 | 9.69 |
| 19:45 | 1635 | BSC Young Boys vs Manchester Utd | 6.69 | 4.64 | 1.44 |
| 19:45 | 1873 | Sevilla FC vs RB Salzburg | 1.66 | 4.19 | 4.59 |
| 20:00 | 1366 | Erzurum BB vs Umraniyespor | 2.28 | 3.23 | 2.89 |
| 20:00 | 5236 | Al Sharjah SC vs AL Wahda Scc (UAE) | 2.20 | 3.50 | 2.82 |
| 20:00 | 5866 | Helsingborg vs Trelleborgs FF | 2.02 | 3.40 | 3.70 |
| 21:00 | 1704 | Walsall vs Brighton U21 | 2.15 | 3.73 | 2.76 |
| 21:00 | 2374 | Leyton Orient vs Southampton U21 | 2.12 | 3.58 | 2.90 |
| 21:00 | 2969 | Morecambe vs Everton U21 | 2.25 | 3.73 | 2.62 |
| 21:00 | 4101 | Tranmere vs Leeds United U21 | 2.15 | 3.74 | 2.77 |
| 21:00 | 4891 | FC Thun vs FC Stade LS Ouchy | 1.71 | 3.88 | 3.98 |
| 21:45 | 1374 | Newport vs Northampton | 2.40 | 3.04 | 2.99 |
| 21:45 | 1396 | Blackpool vs Huddersfield | 2.71 | 3.10 | 2.61 |
| 21:45 | 1866 | Altrincham vs Kings Lynn | 2.05 | 3.56 | 3.17 |
| 21:45 | 2350 | Notts County vs Wealdstone | 1.36 | 4.88 | 7.02 |
| 21:45 | 2707 | Dagenham and Redbridge vs Weymouth | 1.39 | 4.59 | 6.84 |
| 21:45 | 2875 | Southend vs Aldershot | 1.58 | 3.92 | 5.10 |
| 21:45 | 2915 | Sutton United vs Hartlepool | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 21:45 | 2994 | Lincoln vs Rotherham | 2.60 | 3.19 | 2.65 |
| 21:45 | 3362 | Maidenhead U vs Stockport | 3.03 | 3.42 | 2.16 |
| 21:45 | 3520 | Ipswich vs West Ham United U21 | 1.69 | 3.88 | 4.08 |
| 21:45 | 4031 | Solihull Moors vs Torquay | 1.86 | 3.71 | 3.61 |
| 21:45 | 4165 | Chesterfield vs Barnet | 1.31 | 5.08 | 8.01 |
| 21:45 | 4218 | Bournemouth vs QPR | 1.95 | 3.44 | 3.69 |
| 21:45 | 4308 | Boreham Wood vs Halifax | 1.90 | 3.43 | 3.73 |
| 21:45 | 4488 | Airdrieonians vs Alloa Athletic | 2.43 | 3.32 | 2.69 |
| 21:45 | 4547 | Grimsby vs Wrexham | 2.37 | 3.52 | 2.64 |
| 21:45 | 4548 | Sligo Rovers vs Dundalk FC | 2.43 | 3.11 | 2.77 |
| 21:45 | 4648 | Eastleigh vs Dover | 1.55 | 4.12 | 5.10 |
| 21:45 | 4768 | Brackley Town vs Darlington | 1.59 | 4.07 | 4.55 |
| 21:45 | 4849 | Woking vs Bromley | 2.55 | 3.43 | 2.50 |
| 21:45 | 5018 | Sheffield Utd vs Preston | 1.90 | 3.30 | 4.04 |
| 21:45 | 5545 | Blackburn vs Hull City | 2.11 | 3.40 | 3.25 |
| 22:00 | 1172 | Villarreal vs Atalanta | 2.48 | 3.59 | 2.65 |
| 22:00 | 1692 | Chelsea vs Zenit St Petersburg | 1.20 | 6.38 | 14.95 |
| 22:00 | 2980 | Lille vs VfL Wolfsburg | 2.58 | 3.33 | 2.68 |
| 22:00 | 4013 | West Bromwich vs Derby | 1.51 | 4.04 | 6.11 |
| 22:00 | 4306 | Malmo vs Juventus | 5.83 | 4.32 | 1.52 |
| 22:00 | 4385 | Reading vs Peterborough | 2.36 | 3.20 | 2.95 |
| 22:00 | 4696 | Dynamo Kiev vs Benfica | 3.30 | 3.30 | 2.20 |
| 22:00 | 5771 | Barcelona vs Bayern Munchen | 3.40 | 4.00 | 1.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# PIOLI: IBRAHIMOVIC ANA MOTO NDANI YAKE




**MILAN, Italia**

STEFANO Pioli amesema Zlatan Ibrahimovic ana "moto ndani yake" baada ya kurudi uwanjani kutoka kwenye majeruhi na bao moja katika ushindi waliopata AC Milan wa mabao 2-0, dhidi ya Lazio hapo Jumapili.

Ibrahimovic - alirudi uwanjani kwa mara ya kwanza akitoka kuuguza goti aliloumia Mei mwaka huu, akiingia kutoka benchi dakika ya 60 na hakuchelewa kutoa mchango wake, kwani dakika saba baadaye alifunga bao la pili kwa AC Milan.

Walikuwa tayari wanaongoza bao moja shukrani kwa Rafael Leao akifunga bao lake la pili kwa msimu huu, huku penalti ya Franck Kessie ikigonga mwamba kipindi cha kwanza.

Matokeo hayo yameifanya Milan kushinda mechi zake zote tatu za mwanzo za Serie A msimu huu.

Ibrahimovic atafikisha umri wa miaka 40 mwezi ujao, lakini kocha wa Rossoneri hao, Pioli amesema umri wake hautakuwa kizuizi kwa yeye kuendelea kufurahia mafanikio pale San Siro.

"Zlatan hajacheza mechi kwa miezi minne, hivyo nina furaha yeye alifunga bao na anaendelea kuwa imara kwa michezo ijayo," alisema akiiambia DAZN.

"Ana moto ndani yake. Kwa namna anavyopambana kwenye mazoezi pamoja na katika mechi, yote hayo yanamfanya yeye kuwa bora. Huwezi kuhisi kama ana umri mkubwa kwa kile anachokifaya."



# MOURINHO ASHEREHEKEA MECHI YA 1,000 KIAINA YAKE

**ROME, Italia**

JOSE Mourinho amesema atakumbuka sana ushindi wa dakika ya mwisho wa AS Roma, dhidi ya Sassuolo baada ya kusheherekea mechi yake ya 1,000 katika maisha yake ya ukocha.

Sherehe ya Mourinho kufikisha idadi hiyo ya mechi kulimfanya ashangilie kwa staili ya kukimbia hadi katikati ya uwanja wakati Stephan El Shaarawy alipofunga bao dakika ya 91 na kuwawezesha Giallorossi kupata ushindi wa 2-1, Jumapili.

Kocha huyo wa zamani wa Porto, Chelsea, Inter, Real Madrid, Manchester United na Tottenham, Mourinho ameshinda mechi 638 katika maisha yake ya ukocha katika mashindano yote, ikimfanya kuwa sawa na asilimia 64 ya ushindi, huku akibeba mataji 25.

Baada ya Mourinho kushuhudia Roma ikishinda mechi yake ya tatu ya Serie A mwanzoni mwa msimu huu, wapo kileleni mwa msimamo na kocha huyo mwenye umri wa miaka 58, ameelezea jinsi mechi hiyo itakavyokaa kwenye kumbukumbu zake.

"Kwa sababu ndani ya wiki hii nilikuwa nawaongopea watu kwa kuwaambia, hii haitakuwa mechi maalumu kwangu - pengine nilikuwa najaribu kujishawishi mwenyewe," alisema Mourinho, ambaye huu ni msimu wake wa kwanza akiwa na Roma.

"Lakini ukweli ni kwamba, huu ulikuwa mchezo maalumu na wenye maana kubwa zaidi kwangu.

"Nina uhakika mchezo huu nitaukumbuka sana kwenye maisha yangu yote, kwa sababu kufikisha mechi 1,000 kama kocha sio jambo rahisi.

"Sikutaka kupoteza na nilikuwa na hofu sana, kwamba mechi hii naweza kupoteza. Lakini baadaye mambo yalibadilika na ilikuwa furaha kubwa kwangu."

Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu England, LaLiga, Serie A na Ligi Kuu Ureno, Primeira Liga ni miongoni mwa mataji aliyobeba katika kipindi chake cha maisha ya ukocha.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BENZEMA AMPIGIA SALUTI VINICIUS JR

●●●Ni baada ya Mbrazili huyo kuonyesha kiwango bora huku akipachika wavuni...

**MADRID, HISPANIA**

KARIM Benzema amepaza sauti kusifia kiwango cha Vinicius Junior, wakati Real Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Celta Vigo, akimtaja nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kuwa "wa aina yake".

Benzema alikuwa nyota wa mchezo huo akifunga mabao matatu 'hat-trick' na kutoa asisti moja, katika mchezo huo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, uliochezwa, juzi Jumapili.

Lakini Vinicius pia alikuwa nguzo ya Madrid, akifunga bao ambalo asisti ilitoka kwa Benzema huku pia akipata penalti iliyofungwa na Mfaransa huyo na kumfanya afunge mabao matatu kwenye mchezo mmoja wa LaLiga kwa mara ya kwanza tangu Aprili 2019.

Vinicius mara zote alikuwa akiisumbua safu ya ulinzi ya Celta akipiga chenga mara 11, na alikuwa na wakati mgumu msimu uliopita na ilionekana kama anataka kuondoka hapo Madrid.

Baada ya mchezo huo, Benzema alimsifia nyota huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 21 kwamba, kiwango chake kinazidi kuimarika.

"Vinicius ni mchezaji wa aina yake," alisema Benzema akiiambia Movistar.

"Kwa uhakika kabisa napenda kucheza pamoja na yeye, alionyesha kiwango cha hali ya juu kabisa.

"Yeye ni kijana na nazungumza naye mara zote, nikimpa ushauri, sababu najua nini anachokipitia kwa sasa.

"Lakini anatusaidia sana. Ni mchezaji mkubwa na ameonyesha ana uwezo mkubwa wa kucheza hapa Real Madrid."

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA AMTAKA PHILLIPS
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anaitaka klabu hiyo kumsajili kiungo wa kati wa Leeds na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 25, msimu ujao . (**Fichajes**)

### OLMO AGEUKA LULU
BARCELONA inamlenga mchezaji wa RB Leipzig, Dani Olmo, huku Manchester United, Juventus na Bayern Munich zikionyesha hamu ya kumsajili winga huyo mwenye umri wa miaka 23. **(Marca)**

### FOFANA AITAMANI MADRID
MLINZI wa Leicester City na Ufaransa, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 20, amesema Real Madrid ndio klabu kubwa duniani na ni ndoto yake kuichezea siku moja. **(YouTube, via Marca)**

### RODRIGUEZ ALIPOKWAMA
EVERTON ilishindwa kumuuza fowadi wa Colombia, James Rodrigues kutokana na mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki anaolipwa kuwa mkubwa zaidi. **(Football Insider)**

### ISAK ANUKIA ENGLAND
BAADHI ya klabu za England zinamnyatia mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 21, licha ya mchezaji huyo kutia saini kandarasi ya muda mrefu na Real Sociedad. Arsenal na Chelsea awali zilionyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo. **(Fichajes via Teamtalk)**

### SPURS YAMWANIA TIMBER
KLABU ya Tottenham Hotspur imefungua mazungumzo na Ajax kuhusu uwezekano wa kumsajili beki wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 20, Jurrien Timber. **(Todofichajes)**

### BARCA, DEMBELE KUTETA
BARCELONA inapanga kufanya mazungumzo na wakala wa Ousmane Dembele kuhusu kuongeza mkataba mpya na mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, lakini hakuna mkutano uliofanyika hadi sasa. **(Mundo Deportivo)**

### KASSIE AKARIBIA BARCA
NYOTA wa AC Milan, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 24, anaivutia klabu ya Barcelona, lakini vigogo hao wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Liverpool, Tottenham na PSG ili kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Ivory Coast. **(Mundo Deportivo)**

### LUKAKU AFUNGUKA
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Romelu Lukaku amesema ilikuwa ni ndoto yake tangu akiwa na umri mdogo kuona anafunga bao kwenye Uwanja wa Stamford Bridge. Lukaku amekuwa na kiwango bora tangu msimu uliopita.**( BBC)**

### VLAHOVIC SOKONI
MSHAMBULIAJI wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ambaye alizivutia klabu za Tottenham na Atletico Madrid mwisho wa msimu uliopita, yupo katika mazungumzo ya kuongeza mkataba wake na klabu yake ya Florentina**. (Fabrizio Romano)**

### AOUAR AIKATAA ARSENAL
KIUNGO wa Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 23, amepinga mazungumzo yanayomhusisha yeye na klabu ya Arsenal na amesema anataka kuisadia Lyon kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. **(Metro)**

HABARI MICHEZO

## Coastal : Hatoki mtu Mkwakwani

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema moja ya mikakati yao ni kuhakikisha wanavuna pointi zote katika michezo yao ya nyumbani ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

Coastal Union inaendelea na maandalizi yake ya msimu mpya ikiwa chini ya Kocha, Mellis Medo aliyewahi kuinoa timu ya Gwambina FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno alisema wanaamini mpango huo wa kutopoteza pointi nyumbani utawaweka katika nafasi salama, pia wakipambana kuvuna na pointi nyingine za ugenini.

Mgweno alisema wamejipanga kuanza na ushindi katika mchezo wao wa kwanza, ambao watakaribisha Azam FC, ili kuwaongezea ari wachezaji wao katika vita ya kuwania ubingwa wa Bara msimu mpya.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi, tutaanza na Azam FC na hawajawahi kutoka salama katika uwanja huu, sasa hivi tunatafuta mechi mbili au tatu za kirafiki zenye ushindani na uhalisia wa Ligi Kuu, kuhakikisha tunakwenda katika ligi tukiwa vizuri sana," alisema Mgweno.

## Ibungilo, Kirumba FC kucheza fainali

**Neema Emmanuel, MWANZA**

TIMU ya Ibungilo FC imefanikiwa kutinga fainali ya mashindano ya Kombe la Dk. Angeline Jimbo Cup 2021 baada ya kuifunga Mecco mabao 2-0, katika mechi ya hatua ya nusu fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi.

Kwa ushindi huo, Ibungilo sasa itakutana na Kirumba FC katika mchezo wa fainali utakaochezwa Ijumaa asubuhi jijini humo.

Mabao yaliyoipeleka Ibungilo FC katika hatua ya fainali yalifungwa na Eric Etigino dakika ya 43 huku Frederick Yusuf akisindikiza ushindi huo kwa goli la pili lilipopachikwa dakika ya 74.

Nahodha wa Ibungilo, Damas Paul alisema ushindi huo haukupatikana kirahisi au kwa bahati mbaya, ila ulitokana na wao kujipanga na kupambana tangu hatua ya makundi.

Naye nahodha wa Mecco, Said Juma alisema kutokuwa makini katika kutumia nafasi walizozitengeneza ikiwamo penalti ulisababisha wao kupoteza mchezo huo wa nusu fanaili.

# MTIBWA SUGAR YASAKA MBADALA WA HITIMANA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar imesema imeanza mchakato wa kusaka kocha mpya, ambaye atarithi mikoba iliyoachwa na Thierry Hitimana aliyetua kwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivi karibuni, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru aliliambia gazeti hili klabu yao ina maombi ya kazi kutoka kwa makocha mbalimbali na sasa imeanza kuyapitia na kuteua mmoja, ambaye atachukua 'mikoba' ya Hitimana.

Kifaru alisema wanatarajia kufanya mchakato huo kwa umakini kama ambavyo awali walivyomchukua Hitimana, ambaye alikuwa ni miongoni mwa walimu walioomba kazi ya kuifundisha timu hiyo.

"Kusema kweli tumepata pigo sana kuondokewa na Hitimana. Tayari yeye ndiye tuliyemchagua kuwa kocha wa timu yetu, lakini alichotufanyia wote tunakijua. Pamoja na hayo ametuomba msamaha na sisi kama Mtibwa tayari tumemsamehe na tunamtakia kila la kheri kwenye timu yake mpya anayokwenda kufundisha kwa sababu mpira siyo uadui," alisema Kifaru.

Akieleza kilichotokea, Kifaru alisema walimtumia tiketi ya ndege, ili aje nchini akitokea Rwanda na baada ya kutua Dar es Salaam, walimpa nakala ya mkataba, ili aisome kwa sababu alitaka baadhi ya vipengele kwenye mkataba virekebishwe. "Tuliandika mkataba, ili ausome. Akatuambia atakuja mwenyewe, ili kurekebisha vipengele. Akakaa Dar es Salaam kwa sababu ndiyo kuna kambi yetu kwa sasa. Huko ndiko yalikotokea yote yaliyotokea, lakini sisi kama Mtibwa Sugar tunasema yamekwisha, tumempa baraka zote," Kifaru alisema.

Hitimana aliisaidia Mtibwa Sugar kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuwa na msimu mbaya.

Kwa sasa Hitimana ni kocha msaidizi wa Simba na katika klabu hiyo atashirikiana na Didier Gomes na Selemani Matola kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Simba Day, Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha huyo tayari ameshaungana na kikosi cha Wekundu wa Msimbazi, ambacho kimeweka kambi yake jijini Arusha.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati), akikabidhi kombe kwa nahodha wa mabingwa wa mashindano ya Kombe la Bashungwa 2021 timu ya Bugeni FC, baada ya kuibuka washindi dhidi ya Nyabiyonza FC katika fainali ya michuano hiyo iliyochezwa kwenye Wilaya ya Karagwe, mkoani Kagera, juzi Jumapili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia mgeni tamasha la Wanawake

**Na Saada Akida**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Tamasha la Michezo la Wanawake linalotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 16 hadi 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Neema Msita alisema Rais Samia amekubali ombi lao la kuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo, ambalo litashirikisha michezo mbalimbali kwa wanawake.

Msita alisema tamasha hilo litahusisha michezo nane ikiwamo riadha, netiboli, kikapu, kikapu kwa walemavu, michezo ya jadi, soka na ngumi.

"Timu zitakazoshiriki katika michezo hiyo ni pamoja na JKT Mbweni dhidi ya Uhamiaji katika mchezo wa netiboli, JKT dhidi ya Don Bosco Liones katika mchezo wa kikapu, wavu kutakuwa na Jeshi Stars dhidi ya Magereza," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza katika upande wa soka kutakuwa na mechi kati ya Simba Queens dhidi ya Timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (U-20) pamoja na mchezo wa kuvuta na kuruka kamba, kukuna nazi na kunyanyua vitu vizito.

"Katika tamasha hilo kutakuwa na kongamano kwa watoto wakike, kinamama na wadada kwa kutoa mada mbalimbali ikiwamo shughuli za michezo na biashara kwa wanawake," alisema.

Alisema kwa mwaka huu wa kwanza tamasha hilo litashirikisha timu zilizofanya vizuri katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini mwaka unaofuata wataongeza wigo wa washiriki.

# Michezo

Jumanne Septemba 14 2021
Nipashe



Benzema ampigia saluti Vinicius Jr UKURASA 22

## Mamia wamuaga Hans Poppe Dar



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, Ludigija Ng'wilabuzu (kulia), akiwaongoza mamia ya wadau wa soka nchini kumuaga aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba marehemu, Zacharia Hans Poppe, kwenye viwanja vya Karimjee jijini jana. Anayefuatia (mwenye suti nyeusi), ni Rais wa TFF, Wallace Karia. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kikijipanga kujipima na Aigle Noir kutoka Burundi, Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia aliwaongoza wadau mbalimbali wa michezo kumuaga Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Wekundu wa Msimbazi, Zacharia Hans Poppe kwenye viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam jana.

Mbali na viongozi na mashabiki wa klabu mbalimbali za soka nchini waliojitokeza kutoa heshima za mwisho kwa marehemu Hans Poppe akiwamo Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, serikali iliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala jijini, Ludigija Ng'wilabuzu.

Mwili wa Hans Poppe aliyefariki dunia Ijumaa jioni katika hospitali ya Aga Khan utasafirishwa leo na mazishi yake yatafanyika kesho Jumatano kwenye makaburi ya Kihesa, Mkimbizi mkoani Iringa.

Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, aliliambia gazeti hili wako katika maandalizi ya kucheza mchezo mwingine wa kirafiki kabla ya kuwakaribisha TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwenye siku ya Tamasha la Simba Day.

Kocha huyo alisema anajisikia furaha kujiunga na Simba ambayo ni klabu kubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na sasa imekuwa ikiingia kwenye hatua za makundi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema amejiunga Simba ili kuongeza nguvu kwenye benchi la ufundi na lengo lao ni kuingia hatua ya makundi na ikiwezekana kufika hatua ya nusu fainali michuano hiyo ya kimataifa.

Kocha huyo aliongeza anaamini Simba itaendelea kutawala katika soka la Tanzania kama itaendelea kujipanga vyema kwa sababu imeshafanikiwa kulibeba taji hilo kwa mara ya nne mfululizo huku ikibeba taji la Kombe la FA mara mbili mfululizo.

# YANGA: TUTASONGA MBELE AFRIKA

## ●●●Nabi asisitiza bado wamebakiwa na dakika 90 nyingine za...

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo wa kwanza wa hatua ya awali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria, Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi, amesema kikosi chake bado kina nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa.

Yanga ilikubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya wageni hao, hivyo italazimika kupata ushindi wa kuanzia 2-0 katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumapili huko Nigeria.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wachezaji wa Rivers United walikuwa na nguvu na walimiliki vyema mpira hasa katika safu ya kiungo hali iliyopelekea timu yake ipoteze mechi hiyo ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nabi alisema bado wana dakika nyingine 90 za kukutana na Rivers United na watajiimarisha kutorudia makosa katika mchezo huo wa ugenini.

"Tumepoteza mkono mmoja na mwingine umebaki, katika mpira kuna matokeo matatu, basi mpira bado haujaisha, nimeongea na wachezaji wangu tunaenda kupambana ili kusaka ushindi nchini Nigeria," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema wanaamini utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa na mgumu, hivyo ni lazima wasimame katika imani yao ya ushindi kwa sababu itawasaidia kufikia malengo yao ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Mbali na ubora wa wapinzani wetu lakini pia maandalizi yetu hayakuwa mazuri kwa sababu ya muda mfupi wa wachezaji kufanya maandalizi ya pamoja na kucheza mechi za kirafiki.

"Ukiangalia maandalizi yetu hayakuwa imara kama ilivyo kwa wenzetu, tulienda 'pre season' nchini Morocco, tulitumia siku nne, mbili kwenda na mbili kurudi, lakini tukiwa huko tukakutana na changamoto ya homa ya Uviko 19, tukalazimika kurejea nyumbani, baadaye ratiba ikatubana kwa wachezaji kwenda katika majukumu ya timu ya Taifa, tukiwa pungufu tukakosa mechi nyingi za kujipima nguvu," alisema Nabi.

Aliongeza wanatakiwa kukubali hawakuwa na muda wa kutosha wa maandalizi kama ilivyo kwa Rivers United ambao walipata muda wa kujiandaa vyema na kucheza mechi nyingi za kirafiki kabla ya kuja katika mchezo wao huo.

"Niwapongeze wapinzani wetu, nakubaliana na matokeo haya, bado hatujaondolewa katika mashindano kwa sababu tumemaliza dakika 90 za kwanza, mechi itaendelea katika uwanja wa ugenini," Nabi alisema.

Kuhusu mabadiliko aliyoyafanya katika mchezo huo ambapo alimwingiza Yusuph Athuman kuchukua nafasi ya Heritier Makambo na kuingia kwa Saido Ntibazonkiza, nyota hao walibadilisha mchezo na kutengeneza nafasi nyingi za wazi.

"Yusuph alipoingia timu ilibadilika sana, Saido aliongeza kitu, ni mchezaji mzuri ila ukiangalia kwa jinsi ya umri wake huwezi kumpa dakika zote 90 za mchezo kwa sababu ya nguvu na pumzi zake," alisema Nabi.

Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Thabiti Kandoro, alisema matokeo hayo hayajamfurahisha lakini wana imani kocha wao atayafanyia kazi upungufu na hatimaye kuibuka na ushindi kwenye mchezo wa marudiano.

"Tuna imani na benchi la ufundi na wachezaji wetu, kuna uwezo mkubwa wa kwenda kupata matokeo ya ushindi wa mabao mawili na kuendelea katika uwanja wa nyumbani kwao," alisema Kandoro.

Naye Kocha Mkuu wa Rivers United, Ndubuisi Nduka, alisema amefurahi kupata ushindi wa ugenini ambao unawapa faida kubwa kuelekea mchezo wa marudiano.

Nduka alisema kabla ya mechi hiyo walikutana na changamoto ya kuwakosa wachezaji wake tegemeo watatu ambao walikutwa na uviko 19 kabla ya mechi, lakini walipambana na kuhakikisha wanaanza vyema kampeni ya kuwania taji hilo la Afrika.

"Matokeo hayo ya maabara yalituvuruga na hatukukata tamaa, wachezaji walipambana na kufanikiwa kupata ushindi, tunaenda kujipanga kumaliza kazi nyumbani," alisema Nduka.

Wawakilishi wengine wa Tanzania katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Azam FC na Biashara United walianza vyema kwenye michezo yao ya kwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >